# Nipashe

Jumamosi Julai 25, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580293

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Sumaye afichua siri alivyokataa kuteuliwa nafasi uwaziri mkuu

UKURASA 4




UKURASA 11

# MSHTUKO



**MKAPA** afariki dunia Dar, wengi washikwa butwaa, kuzikwa Jumatano Masasi, Kenyatta na Odinga wamzungumzia...

*Endelea uk. 2*

## KIKWETE AANIKA WALIVYOTETA DAKIKA ZA MWISHO HOSPITALINI

UKURASA 2



**1938 - 2020**

**MICHEZO** TUTAKUKUMBUKA ALAMA UWANJA WA TAIFA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## JK aanika walivyoteta na Mkapa dakika za mwisho

**Na Mary Geofrey**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, amesema alimtembelea Benjamin Mkapa hospitalini juzi na kuzungumza naye kwa saa moja.

Amesema katika mazungumzo hayo, alimwombea Mpaka apone haraka, ili kwa mara nyingine amtembelee nyumbani kwake akiwa mwenye afya njema.

"Jana (juzi) jioni nilienda kumwona hospitali, nikaongea naye sana. Ingawa alikuwa na maumivu makali, lakini hakuwa ni mgonjwa yule ambaye ukitoka pale unaweza kusema hali yake ni mbaya," alisema Kikwete.

Aliwataka Watanzania kuendelea kuwa watulivu wakati wa kipindi hiki kigumu na kuwa wastahimilivu huku wakiamini kuwa kifo kinapangwa na Mungu.

"Sisi Waislam tunasema Innalillah Wainnalillah Rajiun, maana yake ni kwamba sisi ni waja wake na kwake tutarejea, ndiyo maana ya maneno yale. Sasa kuhusu tutarejea lini, ni kazi yake Mungu aliyetuleta duniani," alisema Kikwete.

Aliwataka Watanzania kuendelea kumkumbuka Mkapa kwa mema mengi ambayo ameyafanya na kuhakikisha yale aliyoyasimamia na kuyapigia katika kipindi chote cha uhai wake, yaendelezwe kwa manufaa ya taifa.

Mbali na Kikwete, viongozi wengine wa kitaifa waliofika nyumbani kwa familia ya Mkapa jana ni pamoja na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge la 10, Anne Makinda, mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussen Mwinyi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Idd, Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mpanda, Eusebius Nzigilwa.

Wengine ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Paramagamba Kabudi, Mwenyekiti wa CCM Mkoa Dar es Salaam, Kate Kamba, na Mkuu wa Mkoa huo, Abubakar Kunenge.

UDSM WAAHIRISHA MAHAFALI

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa William Anangisye, alitangaza kuahirisha mahafali ya 50 ya chuo hicho, kufuatilia kifo cha Mkapa.

Alisema walipokea taarifa za kifo hicho kwa mshtuko mkubwa na kwamba mahafali hayo yameahirishwa hadi hapo watakapotangaza tena.

Profesa Anangisye alisema wanamkumbuka kwa mambo makubwa aliyofanya Mkapa katika sekta ya elimu ikiwamo kusisitiza elimu inayoendana na mahitaji ya watanzania, ili kuondoka na kadhia wasomi kutafuta ajira maofisini.

Alisema Rais Mkapa aliweka mitaala ya elimu inayowezesha vijana kujiajiri baada ya kuhitimu vyuo vikuu.

Profesa Anangisye alisema pia aliongeza juhudi za Mkapa kufungua fursa katika kupata elimu ya msingi, sekondari na chuo kikuu, kulikosababisha kuanzishwa kwa vyuo vikuu vingi nchini.

Alisema Mkapa katika kuhakikisha vijana wanapata elimu ya juu, Mkapa alianzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ili kutoa fursa kwa vijana kupata elimu.

"Yapo mengi ya kukumbukwa kumuhusu Rais Mkapa, hususani sekta ya uchumi. Kama wanazuoni tumepoteza mwandishi wa vitabu na alikuwa mwepesi kuweka mawazo yake kwa njia ya maandishi," alisema Profesa Anangisye.



Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akimpa pole Mama Anna Mkapa, mjane wa Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa, nyumbani kwa marehemu, Masaki jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mshtuko kifo cha Mkapa

**Na Mwandishi Wetu**

NI mshtuko! Ndivyo ambavyo yeyote anaweza kusema kutokana na kifo cha Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa kilichotokea usiku wa kuamkia jana jijini Dar es Salaam.

Watanzania wengi wameshtuka kupata taarifa za kifo cha kiongozi huyo aliyeongoza nchi kwa miaka 10 huku akiwa ameweka kumbukumbu muhimu juu ya maendeleo ya taifa katika uchumi, siasa na masuala ya kijamii.

Rais John Magufuli, akitangaza kifo hicho usiku wa kuamkia jana, alisema Mkapa alifariki dunia usiku huo hospitalini jijini ambako alikuwa akipatiwa matibabu.

Kiongozi huyo wa nchi aliwataka Watanzania wote kuwa watulivu na wastahimilivu baada ya kupokea taarifa za kuondokewa na mpendwa wao Mkapa.

Baadaye saa nane usiku wa kuamkia jana, Kurugenzi ya Mawasiliano Ofisi ya Rais, Ikulu, ilitoa taarifa ikibainisha kuwa Rais Magufuli ametangaza siku saba za maombolezo ya kitaifa kuanzia jana kufuatia kifo hicho.

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, katika salamu zake za rambirambi, alisema: "Tutamkumbuka daima kwa mchango wake katika taifa letu kwenye nyanja za siasa, uchumi, diplomasia na jamii."

**KUAGWA UWANJA WA TAIFA**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alikuwa miongoni mwa viongozi wa kitaifa waliofika nyumbani kwa Mkapa, Masaki jijini Dar es Salaam kuipa pole familia ya marehemu.

Baadaye alizungumza na vyombo vya habari na kubainisha kwamba maziko ya Mzee Mkapa yatafanyika Jumatano ijayo kijijini kwao Lupaso, Masasi mkoani Mtwara.

Alisema mwili wa kiongozi huyo mstaafu utaagwa kwa siku tatu mfululizo kuanzia kesho hadi Jumanne ambapo siku hiyo ataagwa rasmi kitaifa.

Majaliwa alisema shughuli za kuaga mwili huo zitatanguliwa na ibada itakayoongozwa na Kanisa Katoliki (RC) kuanzia saa nne na baada ya hapo wananchi wataanza kuaga huku akisisitiza kwamba tukio hilo litafanyika mpaka usiku ikiwezekana.

"Jumanne ndiyo itakuwa siku ya kuaga kitaifa mwili wa mpendwa kiongozi wetu Mzee Mkapa. Shughuli zitaanza kwa ibada na baadaye viongozi mbalimbali wa kitaifa na kimataifa wataaga. Watumishi wa umma wataaga hadi saa sita mchana na saa 8:00 mchana mwili utasafirishwa kwa ndege kwenda Masasi kupitia Uwanja wa Ndege wa Nachingwea.

"Uwanja wa Nachingwea uko kilometa 35 kutoka Masasi wakati ule wa Mtwara ni kilometa 110, hivyo tumeona tutumie huo. Lakini viwanja vyote vitatumika," alisema.

Kuhusu maziko, Majaliwa alisema shughuli za kuaga mwili zitaanza asubuhi hadi saa 6:00 adhuhuri na saa 8:00 mchana mwili utahifadhiwa katika nyumba yake ya milele.

Akiwa Masaki, Waziri Mkuu alisema Watanzania walipata mshtuko na familia yake kwa ujumla na hivyo kuwataka kuwa watulivu na kuendelea kumwomba Mungu kwa sababu kifo hicho ni sehemu ya mipango yake.

Alisema serikali inaendelea na maandalizi kwa kutambua kuwa ni kiongozi wa kitaifa kwa kuzingatia kwamba wakati wa uhai wake, Mkapa alikuwa kiongozi wa kitaifa na kimataifa na alikuwa na marafiki wengi duniani.

"Wajibu wetu kama serikali ni kuwasialiana na marafiki wote na taasisi zote, ili kutoa fursa za wao kushiriki kadri wao watakavyoamua.

"Kwa hiyo, kamati ya maandalizi ya mazishi ya serikali inaandaa taratibu zote, tutapata na kwa kushirikiana na familia, tutatoa taarifa ya kitaifa," alisema Majaliwa.

"Baadaye tutatoa taarifa rasmi za wapi mwili wa mpendwa wetu, baba yetu utapumzishwa wapi, tutatoa taarifa rasmi, hizi ni taarifa za awali," alisema Majaliwa.

**KENYATTA AMLILIA**

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, jana alisema anaomboleza kifo cha Rais Mkapa na kutuma salamu za rambirambi kwa Rais Magufuli.

Rais Kenyatta alimwelezea Mkapa kama kiongozi aliyejituma bila kuchoka kuleta maendeleo ya Ukanda wa Afrika Mashariki, taarifa ya Ikulu ya Kenya ikisema:

"Katika ujumbe wake wa faraja, Rais Kenyatta ameomboleza kifo cha kiongozi wa Tanzania, aliyekuwa kiongozi bora Afrika Mashariki, aliyefanya kazi bila kuchoka kwa ajili ya usuluhishi, amani na maendeleo."

Kiongozi wa Chama cha Upinzani Kenya cha Orange Democratic Movement (ODM), Raila Odinga, pia alisema anaomboleza kifo hicho, akisema Mkapa alikuwa rafiki mkubwa wa wananchi wa Kenya.

Alisema Wakenya watamkumbuka Mkapa kutokana na juhudi zake za kuleta amani nchini mwao akishirikiana na Dk. Koffi Annan na Graca Machel, baada ya taifa hilo kukumbwa na machafuko ya kisiasa, yaliyotokana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2008.

"Mkapa aliamini katika ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Afrika imepoteza mtu mkubwa, maombi yangu yako kwa familia yake, Rais Magufuli na watu wa Tanzania," aliandika Odinga katika ukurasa wake wa Twitter.

**KUHUSU MKAPA**

Mkapa alizaliwa Novemba 12, 1938 Ndanda wilayani Masasi mkoani Mtwara. Alipata shahada yake ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda mwaka 1962 na mwaka mmoja baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha Columbia alikopata shahada ya pili katika uhusiano wa kimataifa.

Nafasi alizowahi kuzishika mbali na urais wa Tanzania, ni pamoja na ofisa wa utawala Dodoma na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje kutoka 1977 hadi 1980 na kutoka 1984 hadi 1990.

Mwaka wa 1995, Mkapa alichaguliwa Rais wa Tanzania, msingi wake ukiwa kampeni maarufu ya kupambana na ufisadi iliyoungwa mkono na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

**KITABU CHA MKAPA**

Novemba 12 mwaka jana, Mkapa alizindua kitabu alichokipa jina la 'My Life My Purpose' (Maisha Yangu Kusudio Langu), akifafanua kwa kina maisha yake, uongozi wake na mtazamo wake kuhusu mambo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Miongoni mwa mambo muhimu aliyoyaangazia katika kitabu hicho, ni utitiri wa vyama vya siasa nchini, ambao amesisitiza ni ishara mbaya kwa demokrasia nchini kwa kuwa vyama vingi vimekuwa vikitumiwa vibaya kwa lengo la kunufaisha wachache kiuchumi.

Kupitia kitabu hicho, Mkapa anajutia uamuzi wake katika baadhi ya mambo, ikiwa ni pamoja na hatua zilizochukuliwa kudhibiti machafuko ya kisiasa Zanzibar wakati wa uongozi wake.

Katika kitabu chake hicho, Mkapa pia anazitaka nchi za Afrika, hasa zilizoko kusini mwa Jangwa la Sahara, kuwa na sera imara kuhusu idadi ya watu, akisisitiza kuwa kasi ya kuzaana iliyopo kwenye nchi hizo kwa sasa itakuwa na madhara makubwa miaka ijayo.

# Mkapa auweka kando uteuzi mgombea urais wa CHADEMA

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeahirisha kutangaza uteuzi wa mgombea wake wa urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, kutokana na kifo cha Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa.

Kwa mujibu wa taarifa ya chama hicho iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari, mkutano wa chama hicho na waandishi wa habari kuhusu kutangaza uamuzi wa Kamati Kuu uliokuwa ufanyike jana, umeahirishwa baada ya kutangazwa kwa kifo cha Mkapa.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya CHADEMA, Tumaini Makene, miongoni mwa mambo yaliyokuwa yamejadiliwa katika mkutano huo wa Kamati Kuu mbali na kupendekeza jina la mgombea urais, ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya ilani za uchaguzi mkuu Tanzania Bara na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Waliojitokeza kutia nia katika mchakato wa kuwania urais ndani ya chama hicho kwa mwaka huu, ni pamoja na Makamu Mwenyekiti wa chama, Tundu Lissu na Wakili Simba Akaro. Wengine ni Dk. Mayrose Majinge, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu, Wakili Gaspar Mwalyela, aliyekuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita na Leonard Manyama.

KUTABIRI KIFO

Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, alisema jana kuwa Rais Mkapa alimhakikishia hatafikisha umri wa miaka 86 alipokuwa na umri wa miaka 70, akidai kuwa aliona umri wa miaka 80 unakuwa wa tabu na msongo wa mawazo.

"Ni kweli hakufikisha ambavyo alinitamkia, msiba wa Mkapa umetokea ghafla, ingawa mwenyewe alitabiri kifo chake mwenyewe," alisema Mbatia na kubainisha kuwa Mkapa ameacha zawadi kubwa ya maisha yake kupitia kitabu chake cha 'My Life My Purpose'.

"Ni baba wa mageuzi kwa sababu ndiye aliyechukua madaraka kwa mara ya kwanza kwa mfumo wa vyama vingi, serikali yake tangu 1995 hadi 2005 alihakikisha mfumo huu unaendelea kwa kutushirikisha kwa kuzungumza na chama kimoja kimoja au vyama vyote ili kuwa na mawazo shirikishi," alisema.

MAPENZI KWA CCM

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alisema anamtambua Mzee Mkapa kama mtu aliyekipenda CCM na aliyekuwa tayari kuilinda kwa nguvu za ziada. "Sina maneno ya kutosha kuelezea kushtushwa kwangu, na nina hakika kwa Watanzania wengi kwa kupata taarifa za mzee wetu, kiongozi wetu na alama mojawapo muhimu kwa taifa letu, Mzee Mkapa kutangulia mbele ya haki," alisema.

Mbowe alisema kupitia maisha yake, Mkapa ameacha alama ya uongozi kwa taifa kupitia nafasi mbalimbali za utumishi wa umma alizoshika wakati wa maisha yake kuanzia wakati wa serikali ya Rais wa Kwanza ya Nyerere.

KAULI YA ACT-WAZALENDO

Chama ACT-Wazalendo katika taarifa yake iliyotolewa na Kaimu Katibu Mkuu, Joran Bashange, kilisema msiba huo ni mzito kwa taifa kutokana na mchango wake mkubwa aliotoa kwenye utumishi wake. "Tunamkumbuka Rais mstaafu Mkapa kama kiongozi aliyeacha alama ya kiuongozi kwenye maeneo mbalimbali hasa katika vita ya kupambana na rushwa na ufisadi, kuanzisha misingi imara ya kujenga uchumi kwa kuruhusu sekta binafsi kuchangia uchumi wa taifa.

"Kusimamia mapato ya kodi, kujenga uhusiano mzuri wa kidiplomasia ikiwamo kusuluhisha migogoro ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla," taarifa hiyo ilisema.

UJASIRI WA MKAPA

Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahim Lipumba, alisema Rais mstaafu Mkapa atakumbukwa kwa ujasiri wake wa kukiri na kujuta kutokana na upungufu uliojitokeza wakati wa utawala wake. Kupitia taarifa yake, alisema Rais mstaafu Mkapa aliisaidia Tanzania kufanya mapinduzi madogo ya kiuchumi na uwekezaji na ni katika utawala wake nchi ilisamehewa madeni makubwa kutoka mataifa tajiri.


iPP CARES FOR YOU

**Uongozi na Wafanyakazi wa Makampuni ya IPP umepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Rais Mstaafu wa awamu ya tatu Mh.Benjamin William Mkapa.**

**Tunatoa pole zetu za dhati kwa Mama Anna Mkapa na familia, Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Watanzania wote kwa ujumla. Mwenyezi Mungu atupe uvumilivu katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.**

**#RIPMkapa**

# Sumaye afichua siri zake na Mkapa

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kutangazwa kwa kifo cha Rais wa serikali ya awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, usiku wa kuamkia jana, Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye, amesema ameshtushwa na kifo hicho na kueleza kuwa Mkapa alikuwa hazina kwa taifa, Afrika na dunia kwa ujumla.

Sumaye ambaye amepata nafasi ya kuhudumu katika nafasi ya Waziri Mkuu katika miaka yote 10 ya utawala wa serikali ya awamu ya tatu chini ya Rais Mkapa, pia amebainisha namna ambavyo aliaminiwa na kufanya kazi zake bila kusumbuliwa na Mkapa.

Akizungumza zaidi kuhusu kifo cha Mkapa, Sumaye alisema jana kuwa: "Kwa kweli taarifa ya kifo cha Mzee Mkapa, Rais mstaafu wa awamu ya tatu imekuwa ya kushtua kwa kila Mtanzania kwa sababu tunamfahamu Mzee Mkapa vizuri.

"Lakini, mimi ambaye nimefanya naye kazi kwa miaka 10 kama Waziri Mkuu wake, kwa kweli imenigusa sana kwa sababu mzee huyu alikuwa hazina kubwa sana kwa taifa letu, hazina kwa Afrika na hazina kwa dunia.

"Alijijengea heshima, aliijengea nchi yetu heshima wakati wa kipindi chake, hakika alifanya kazi kubwa ambayo Watanzania wote wanaikumbuka na wanaielewa."

Sumaye alisema Mkapa alimteua kwa awamu zote mbili za urais wake kuwa waziri mkuu, akisisitiza kuwa hiyo ilimaanisha alikuwa na imani kubwa kwake.

"Nilikuwa ninafanya kazi kwa uhuru, kwa amani na kufanya kazi bila woga wowote," alisema.

MAJANGA, AJALI

Akimwelezea zaidi Mzee Mkapa, Sumaye pia alizungumzia mambo mengi zikiwamo nyakati ngumu ambazo utawala wa serikali ya awamu ya tatu ulipitia.

Kwa mujibu wa Sumaye, katika utawala wowote kuna mambo mengi yanatokea, hivyo walitarajia pia kukutana na nyakati hizo ngumu.

"Kama utakumbuka wakati wa utawala wake, ndipo ambapo nchi ilikuwa inaingia kwenye mageuzi mengi, ni Mkapa ndiyo aliingiza nchi kwenye mageuzi mengi ya kiuchumi, ndiyo tulikuwa tunabadilisha sasa kuingia kwenye mfumo wa biashara huria.

"Tulifanya marekebisho ya utumishi wa umma kama mnakumbuka, watu wengi ilibidi wapunguzwe serikali ili kupata idadi ya watu ambao inaweza kuwa sahihi, kulikuwa na ajali nyingi zilitokea kama ajali ya meli MV Bukoba na hata kifo cha Mwalimu Julius Nyerere.

UKALI WA MKAPA

Akimzungumzia utendaji kazi wa Rais Mkapa, Sumaye alisema: "Ukali wa Mzee Mkapa nilikuwa ninaujua na nilikuwa ninaupenda kwa sababu mimi mwenyewe nilikuwa ninapenda kiongozi mkali kwa yale mambo ambayo yanaonekana siyo sahihi.

"Ukali wa Mkapa haukuwa tu hauna mpangilio, kwa Mkapa kama unafanya kazi vizuri hamuwezi kugombana na wala huwezi kuona ukali wake, lakini kama unafanya kazi vibaya mtagombana tu.

"Kwa hiyo ni ukali mzuri, ukali ambao unarekebisha mambo, ukali ambao hauzuii kufanya mazuri ambayo unataka kuyafanya katika nafasi yako ya utumishi," Sumaye alisema.

KUUKATAA UWAZIRI MKUU

Sumaye mbali na kueleza namna alivyoaminiwa na Rais Mkapa kwa kumteua kuwa Waziri Mkuu wake kwa kipindi cha miaka 10, pia alifichua alivyomkatalia kiongozi huyo kumteua kutumikia nafasi hiyo kubwa.

"Kama nikitaka kueleza ukweli kabisa, sikuwa na mazoea naye ya karibu, sikutegemea kupata nafasi ya waziri mkuu, aliponiteua nilimkatalia na kumwambia ampe mtu mwingine, lakini naye alikataa.

"Baada ya kumalizika kwa miaka mitano na kujiandaa kwa awamu ya pili, nilimuaga vizuri nikamwambia ninaomba safari ijayo umtafute waziri mkuu mwingine, nikamweleza changamoto zilizopo, akanielewa, lakini tuliporudi tena akaniteua tena, lakini nikamwambia 'nilishakuomba mimi nisiwe waziri mkuu'. "Akanijibu lazima uendelee. Kwa hiyo, mimi ni mtu ambaye utaona anakuteua siyo kwa sababu mnafahamiana, au kuna mtu ameenda kukusemea, bali alikuwa anateua kwa jinsi yeye anavyokuona.



Waziri Mkuu mstaafu John Malecela akizungumza na waandishi wa habari, nyumbani kwake, jijini Dodoma jana, kuhusu jinsi alivyomjua Rais mstaafu marehemu Benjamin William Mkapa, enzi za uhai wake. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## TAMWA yakumbuka mchango wake katika usawa wa jinsia

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimesema kinaungana na Watanzania wote kuomboleza kifo cha mwanadiplomasia mkongwe, mwanahabari mahiri na Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, TAMWA ilisema inakumbuka mchango wa Mkapa katika kuijenga nchi kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni lakini hasa katika kujenga na kuhimiza usawa kijinsia, kisheria, kisera na katika ngazi za uamuzi.

Mmoja wa waanzilishi wa TAMWA, Eda Sanga, alisema anaukumbuka mchango wa kiongozi huyo katika kusimamia ubora wa habari, usawa wa kijinsia hasa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya Sospa ya mwaka 1998.

"Mimi binafsi nimefanya naye kazi kwa ukaribu kabisa. Nikiwa nafanya kazi RTD (Radio Tanzania Dar es Salaam-sasa TBC Taifa), yeye alikuwa anasoma taarifa ya habari na mimi nikisimamia vipindi vya 'External Service'," alisema.

"Huyu ndiye alikuwa waziri wetu wa habari, wakati tunaanzisha TAMWA. Mimi nikiwa na wenzangu tulienda ofisini kwake tukiwa na nakala ya jarida la 'Sauti ya Siti', tulimpa ili alione asije tu kuliona mtaani. Tukaongea naye, ili akubaliane na yale tuliyotaka, kwa sababu wakati huo tulikuwa ni waandishi wa vyombo vya habari vya serikali.

"Huyu baba alisaidia sana kuwaona wanawake katika sura hiyo mpya, sura ya kufanya taifa liwe na usawa wa kijinsia, kwa kuwa sote tunaamini kuwa taifa likiwa na wanaume peke yake, ni sawa na mtu anayekwenda na mguu mmoja."

Mwanzilishi mwingine wa TAMWA, Rose Haji Mwalimu, alisema anamkumbuka Mkapa wa kupambana na kumaliza mauaji ya vikongwe.

"Rais Mkapa tunamkumbuka kwa mengi, alikuwa mstari wa mbele, hasa katika kutetea haki za jinsia, ameongeza idadi ya wanawake katika uongozi na kumaliza mauaji ya vikongwe," alisema.

"Kwa kweli ni pigo kubwa kwa TAMWA kupoteza nguli huyu wa habari kutokana na mchango wake katika masuala ya jinsia, nashauri TAMWA tungefanya mkesha kumuenzi jemedari huyu."

# Watu mashuhuri wamlilia Rais Mkapa

**Na Waandishi Wetu**

MFANYABIASHARA maarufu na tajiri namba moja nchini, Mohammed Dewji 'MO', na watu mashuhuri, wameeleza namna walivyoguswa na kifo cha Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa.

Kwa mujibu wa Rais John Magufuli aliyetangaza taarifa za kifo hicho, Mkapa aliyezaliwa mwaka 1938, alifariki dunia usiku wa kuamkia jana jijini Dar es Salaam.

Baada ya kutangazwa kwa kifo hicho, MO Dewji, miongoni mwa mabilionea vijana barani Afrika, aliandika kwenye ukurasa wake rasmi wa Twitter akisema:

"Bado ni ngumu kukubali kwamba Mzee Mkapa hatunaye tena. Pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa ujumla kwa msiba huu mzito. Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi, Tangulia Baba, nasi tunakuja."

WAZIRI KIGWANGALLA

Aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, pia aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter akisema: "Nimepokea msiba wa Mzee Benjamin William Mkapa kwa masikitiko makubwa sana. Ninatuma salamu za pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki na Watanzania wenzangu wote, pumzika kwa amani baba yetu."

JANUARY MAKAMBA

Aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Mbunge wa Bumbuli mkoani Tanga katika Bunge lililopita, January Makamba, alisema:

"Bado ni vigumu sana kuamini kwamba Mzee Mkapa hayunaye tena. Pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote. Ni msiba mzito kwa taifa letu, Mwenyezi Mungu amlaze pema peponi."

WAZIRI UMMY

Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, alisema: "Ni majonzi makubwa kwa Tanzania. Tumwombee mzee wetu Rais mstaafu Benjamin Mkapa apumzike kwa amani.

"Ninatoa pole kwa mke wa marehemu, Mama Anna Mkapa, watoto, familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzani wote. Bwana na ametoa, bwana ametwaa."

JOKATE MWEGELO

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, alisema: "Nimepokea taarifa za kifo cha Mzee wetu Rais wa awamu ya tatu, Ndugu Benjamin William Mkapa kwa masikitiko makubwa sana.

"Salamu zangu za pole ziende kwa Watanzania wote. Mzee Mkapa alikuwa ni baba, mwalimu, mlezi na wengi tulimtazama kama kioo. Binafsi nimejifunza mengi kupitia uongozi wake na maisha yake kwa ujumla.

"Tunashukuru kwa kutuacha na kitabu cha maisha yako kitakachobaki kama kumbukumbu na sehemu ya sisi kujifunza na vizazi vijavyo. Pumzika kwa amani mzee wetu."

JAJI WARIOBA

Waziri Mkuu mstaafu na jaji mstaafu, Joseph Warioba, alisema: "Mwaka 1995, Rais Mkapa alikuwa ananiambia mimi nigombee na mimi nikawa ninamwambia 'hapana wewe ugombea'.

"Kila mmoja akagombea, kila mmoja na mtandao wake, lakini tukasema tutashirikiana. Wakati wa kutafuta wadhamini, mtandao wake na wangu ukashirikiana.

■ Imeandikwa na Mary Mshami, Magdalena Haule, Fatma Mtutuma na Faudhia Sultan




# TANZIA

Mwenyekiti wa Baraza, Makamu Mkuu wa Chuo, na Jumuiya nzima ya Chuo Kikuu cha Dodoma tumepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, **Mhe. Benjamin William Mkapa** kilichotokea usiku wa kuamkia leo tarehe 24 Julai, 2020. **Mhe. Mkapa** amekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma tangu kilipoanzishwa mwaka 2007 mpaka umauti ulipomkuta.

Katika uongozi wake amekuwa nguzo muhimu katika maendeleo ya Chuo. Atakumbukwa kwa mengi ikiwa ni pamoja na kuunganisha Chuo na wadau mbalimbali kutoka Japan waliowezesha usafishaji wa damu (dialysis) katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Wadau hao pia walisaidia upandikizaji wa figo katika Hospitali ya Rufaa ya Benjamin Mkapa kwa ushirikiano na madaktari wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Chuo kinatoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Familia ya Marehemu, Jumuiya ya Chuo na Watanzania kwa ujumla kwa msiba huu mzito.

**Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu, Benjamin William Mkapa mahali pema peponi.**



**MHE. BENJAMIN WILLIAM MKAPA**
**1938-2020**

Raha ya milele umpe ee Bwana na mwanga wa milele umuangazie.

**-Apumzike kwa amani-**

THE UNIVERSITY OF DODOMA
UDOM
Embracing Knowledge

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Buriani Mkapa, alama yako sekta ya michezo haitafutika

**WATANZANIA** na Taifa kwa ujumla wapo katika majonzi makubwa baada ya kuondokewa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa, aliyefariki dunia usiku wa kuamkia jana hospitalini jijini Dar es Salaam alipokuwa amelazwa kwa matibabu.

Ni awamu nyingi zimekuja na kupita kuanzia ya kwanza chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ikaja ya pili ikiongozwa na Ali Hassan Mwinyi ya tatu ya Mkapa na kisha ya nne chini Jakaya Mrisho Kikwete na sasa hii ya tano ya Rais John Pombe Magufuli.

Tukiiacha hii ya tano ambayo, Rais Magufuli anaendelea kufanya mengi makubwa akiendelea kuweka alama kubwa katika Taifa la Tanzania, watangulizi wake wamefanya makubwa hadi alipopokea kijiti hicho kutoka kwa Kikwete.

Hakuna anayeweza kumnyooshea kidole Muhasisi wa Taifa hili, Mwl. Nyerere hasa kwa juhudi zake za kututoa katika ukoloni na kufanya makubwa mengi ambayo yaliendelezwa na Mwinyi, Mkapa, Kikwete na sasa Magufuli.

Pamoja na hayo yote, Nipashe tunachukua fursa hii kuungana na Watanzania katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na Rais wetu mpendwa Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa ambaye ametimiza safari yake hapa duniani usiku wa kuamkia jana. Kuna mengi makubwa mazuri na alama nyingi alizoziacha Mkapa ambazo tukianza kuzielezea zinaweza kujaza ukurasa wa kwanza hadi wa mwisho wa gazeti hili na bado lisitoshe kuzibeba.

Hata hivyo, kwa kuanza tumevutiwa kugusia angalau kwa uchache mengi aliyoyafanya katika sekta ya michezo na alama kubwa aliyoiacha kwa Taifa hili ambayo itabaki kukumbukwa vizazi hadi vizazi. Kwanza wanamichezo na Watanzania kwa ujumla leo hii tunatembea kifua mbele kwa kuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza barani Afrika kwa kuwa na uwanja bora kabisa wa michezo, tukijivunia Uwanja wa Taifa uliofunguliwa rasmi mwaka 2007 ukibeba watazamaji 60,000.

Hiyo ni alama kubwa iliyowekwa na Hayati Mkapa ambaye alikerwa kuona Watanzania wakishindwa kulifurahia soka kutokana na msongamana katika Uwanja wa Uhuru uliojengwa tangu mwaka 1961 ukichukua watazamaji 23,000 pekee.

Sote tunakumbuka namna Watanzania walivyokuwa wakikosa nafasi ya kuhudhuria mechi kubwa kutokana na udogo wa uwanja husasan Simba na Yanga zilipocheza, lakini leo tatizo si uwanja tena bali ni juhudi za kuhamasisha mashabiki kuhudhuria kwa wingi ili kuujaza, hakika Mkapa tutakukumbuka daima.

Alama hiyo inaonyesha ni kwa namna gani Mkapa alikuwa mwanamichezo wa kweli na ambaye alitamani kuiona Tanzania ikipiga hatua kubwa katika sekta ya michezo kimataifa.

Aidha, tunakumbuka juhudi za Mpaka pia alipomaliza tofauti iliyokuwapo ndani ya Chama cha Soka nchini (FAT) kwa sasa Shirikisho la Soka nchini (TFF), na kusababisha kufungiwa na Fifa, enzi ikiwa chini ya Mwenyekiti, Muhidini Ndolanga na Katibu Mkuu, Ismail Aden Rage.


Juhudi za Mkapa zilisaidia Tanzania kurejeshewa uanachama wa Fifa baada ya kumaliza tofauti iliyokuwapo FAT enzi hizo, hakika ni mengi amelifanyia soka letu ikiwa ni pamoja na nyakati tofauti serikali yake kuweka mkono kwa kuisaidia timu ya Taifa, Taifa Stars pindi ilipokwama kwenda kushiriki michuano ya kimataifa kutokana na ukata.

Mkapa alikuwa mwanamichezo wa kweli na katika uongozi wake hadi anaaga dunia pamoja soka la Tanzania kutawaliwa na ushabiki wa Simba na Yanga, sote tutakubali kwamba hakuonyesha kuegemea upande wowote jambo ambalo limewaacha wengi wakiwa hawafahamu alikuwa mpenzi wa klabu gani kati ya hizo mbili. Buriani Mkapa, tutakukumbuka daima katika jitihada zako za kulijenga Taifa, na katika kipindi hiki, tunaungana na familia yake na Watanzania wote kumuomba Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi. Hakika Tulikupenda ila Bwana Alikupenda Zaidi, Jina lake la Bwana Libarikiwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Morrison asizalishe virusi Yanga!

Na Barnabas Maro

**'VIRUSI'** ni viini vinavyosababisha ugonjwa; pia ni programu za kompyuta zinazoharibu faili. *Viini ni wingi wa 'kiini' na maana yake ni sehemu zilizo ndani kabisa ya vitu kama vile watu au mayai; aidha, ni vyanzo vya vitu; kadhalika, ni sababu ya kutokea mambo na asili zake.

Mchezaji Morrison aliyesajiliwa na Yanga akitokea kwao Ghana, ni kirusi kwa wachezaji aliowakuta klabu ya Yanga. Cha kushangaza ni viongozi wa klabu kutochukua hatua mujarabu (-enye kufaa kutibia maradhi; chenye kufaa kutengenezea jambo au kutatulia tatizo) dhidi yake. Wamwache aende atakako kwani kadiri wanavyom-bembeleza, ndivyo anavyodhani kuwa yeye ndiye kila kitu, si kwa wachezaji tu bali hata kwa viongozi wa klabu!

Kwa nini Morrison anadekezwa kiasi hiki? Anadhani yeye ni muhimu zaidi ya wote aliowakuta na ambao hucheza kabumbu katika timu ya wachezaji 11 uwanjani? Wenzake wakikata tamaa na kutocheza kwa ari ili kumwachia afanye atakalo uwanjani, atafanya mbwembwe (mikogo) zake bila ushirikiano na msaada wa wenzake? 'Mchezo' ni jambo ambalo watu au timu hufanya kwa kushindana ili kupata mshindi; pia ni jambo linalofanywa kwa nia ya kuburudisha. Kama wachezaji hawana umoja uwanjani hakuna tegemeo la ushindi kwani "kidole kimoja hakivunji chawa," chambilecho wahenga.

Tangu Yanga ilipoundwa mwaka 1935, imekuwa na wachezaji wengi hodari kuliko Morrison na hawakuwa na kiburi wala kujiona bora kuliko wengine. Seuze yeye? Kadiri viongozi wa Yanga wanavyokuwa kimya ndivyo mkaidi Morrison anavyozidi kuvimba kichwa, kuwakatisha tamaa wachezaji wenzake, na kulitawala benchi la ufundi na viongozi sawia (kwa wakati mmoja)!

Kwa nini viongozi wanakuwa kimya katika hali inayowakatisha tamaa wachezaji, wanachama na mashabiki wa klabu? Ameikuta timu inayoitwa Yanga na ataiacha ikiitwa jina hilo hilo - Yanga, si Morrison! Akafanye kiburi (hisia ya kujiona na kujivuna) huko aendako aone kama atavumiliwa. Hebu (tamko la kumtaka mtu akusikilize) azingatie methali isemayo: "Tamu ikizidi tamu huwa si tamu tena." Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba jambo lolote zuri huwa na mipaka lakini linapozidi huwa halivutii tena.

Ole! (tamko linalotumika kuonesha kujutia jambo hasa baya) Morrison kwani hata wahenga walituachia methali isemayo: "Mwenye pupa hadiriki kula tamu." Pupa ni nia ya kutaka kufanya jambo kwa haraka. Maana yake anayekula chakula kwa kukipapiapapia hawezi kuufaidi utamu wake.

"Mwenye kushiriki moyo asourudi mtima, hufa maji pondo-ima, na kuondoka na kilema." Maana yake yeyote anayekubali matakwa ya moyo wake bila ya kuukanya, hufa kwa kuzama katika maji ya kina kifupi na kuondoka na fedheha. Methali hii yatunasihi umuhimu wa kuikanya mioyo yetu. Tusiwe na tabia ya kufanya jambo lolote ambalo moyo unatamani.

Hii ni methali ya kuwanasihi watu kutokuwa na tabia ya kufanya mambo kwa papara (ukosefu wa umakini katika kufanya jambo) na pupa (tabia ya mtu kuwa na haraka bila ya mazingatio ya kujua, kupata au kusema jambo) kwa kuwa aghalabu matokeo yake huwa mabaya. Morrison anapaswa kufikiri mara mbili na kwa wanaotaka kumchukua, wafanye tafakuri tunduizi (-a muhimu sana; -enye undani, -enye uzito na dharura ya kufanyika). Vinginevyo yatawapata kama yanayowapata Yanga sasa!

Morrison ana tamaa ndo maana hakai na timu moja kwa muda mrefu. Kila alikokuwa hakuondoka kwa heri, yaani utulivu na salama; hali ya kupata baraka na mafanikio. "Tamaa mbele mauti nyuma." Maana yake ukiiweka tamaa mbele, mauti yatakuwa nyuma yakikufuata, mabaya yatakupata. Methali hii hutumiwa kwa mtu mwenye tamaa nyingi. Twafunzwa madhara yanayoweza kutupata kutokana na tamaa isiyokuwa na mipaka. Morrison hapaswi kuwa mchezaji wa timu yoyote Tanzania. Aondoke, asituachie 'virusi vyake'.

Timu ijengwe upya kwani hali ilivyo sasa, viongozi wa klabu, kocha na usajili wa wachezaji hairidhishi. Kocha Eymael anaonekana kutaka kuwatoa wasaidizi wake akiwamo aliyekuwa kocha kabla yake, Boniface Mkwasa, na kocha Peter Manyika wa makipa, waliokuwa wachezaji wa zamani wa Yanga, kwa kujiona yeye ni kocha mweledi.

Huenda viongozi hawajui jinsi ya kuongoza klabu ya kandanda kwani ni kama wamekabidhi madaraka na shughuli zote kwa Kampuni ya GSM inayoifadhili klabu kwa kusajili wachezaji wanaopendekezwa na kocha, usafiri wa wachezaji na kulipa mishahara.

Eymael naye anapaswa kuondoshwa kwani pamoja na kujipambanua kama kocha 'mweledi' hakuna weledi anaouonesha tangu akabidhiwe timu ya Yanga! Labda 'weledi' anaojivunia ni kupiga kelele uwanjani tangu mwanzo mpaka mwisho wa mchezo. Anashindwa kuwaelekeza wachezaji wajibu wao wanapokuwa mazoezini? Wapo makocha wengi Watanzania wenye weledi kuliko yeye mtoka mbali.

MKAPA 1938 - 2020

# MSIBA WA RAIS MSTAAFU MZEE BENJAMINI WILLIAM MKAPA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimpa pole Mama Anna Mkapa, Mjane wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa, nyumbani kwa marehemu, Masaki jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**



Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambaye ni mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Mwinyi, akitia saini kwenye kitabu cha maombolezo nyumbani kwa marehemu. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mwenyekiti wa Chama cha NCCR – Mageuzi Taifa, James Mbatia (kulia), akisalimiana na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda walipokutana msibani, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Spika mstaafu Mzee Pius Msekwa akitia saini kitabu cha maombolezo. Kulia ni mkewe Mama Anna Abdallah. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waombolezaji wakimfariji Nico Mkapa (mwenye miwani), ambaye ni mtoto wa marehemu. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi akitia saini kitabu cha maombolezo nyumbani kwa marehemu jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TAKUKURU yaokoa mamilioni toka ujenzi wa bwawa la umeme Rufiji

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro imeokoa zaidi ya Sh. milioni 498 kutoka katika kampuni inayofanya kazi kwenye ujenzi wa mradi wa umeme Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Kampuni hiyo ilibainika kutolipa kodi kwa wakati kinyume cha sheria katika Halmashauri za Morogoro na Rufiji ambako mradi huo unatekelezwa.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa taasisi hiyo katika kipindi cha miezi mitatu, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro, Janeth Machulya, alisema ucheleweshaji wa fedha hizo za ushuru wa huduma kutoka kampuni ya Sinohydro Corporation Limited-Rufiji Project, ni kinyume cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982.

Alisema sheria hiyo inazitaka kampuni zinazofanya biashara kutoa tozo ya kiwango cha asilimia 0.3 ya mauzo yake ghafi baada ya kuondoa kodi stahiki huku akibainisha miongoni wa sababu zinazofanya ucheleweshwaji ni ufatiliaji hafifu wa baadhi ya watendaji katika halmashauri husika.

"Baada ya ufuatiliaji, kampuni hiyo ilifanya malipo ya Sh. milioni 211.9 kwa Halmashauri ya Wilaya Morogoro na Sh. milioni 211.9 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa kuwa eneo la mradi linagusa sehemu zote mbili na mchakato wa malipo ya adhabu unaendelea," alisema Machulya.

Alisema ufatiliaji huo pia umesaidia kupatikana malipo ya zaidi ya Sh. milioni 74.8 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ambayo pia yalikuwa yamecheleweshwa kutokana na kutofuatiliwa na watendaji wake.

Katika hatua, TAKUKURU imeokoa Sh. milioni 19.5 za programu ya lipa kulingana na matokea katika sekta ya elimu zilizokuwa zimefujwa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu wa idara ya elimu ya Manispaa ya Morogoro.

"Katika kipindi hiki pia tumefanikiwa kuokoa fedha hizo ambazo zilikuwa zimefujwa na baadhi ya watumishi. Fedha hizi zilikuwa katika mradi wa Education Program for Results na watuhumiwa tunaendelea kuwahoji," alisema.



Mwonekano wa daraja la Kibamba lililoko njia panda ya Mloganzila, jijini Dar es Salaam jana, lililojengwa katika kazi ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa upanuzi wa Barabara ya Morogoro, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha mkoani Pwani yenye urefu wa kilomita 19. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kampuni za mafuta zalalamikiwa makato nje ya kodi za serikali

**Na Joseph Mwendapole**

WAUZAJI wa mafuta wa rejareja, wameibua malalamiko dhidi ya kampuni kubwa za mafuta kwa kuwakata fedha ambazo ni kinyume cha kanuni na hazitambuliwi na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Gazeti hili lilizungumza na wauzaji wa mafuta wa maeneo mbalimbali nchini ambao walisema fedha hizo zimekuwa zikikatwa kwenye mafuta wanayouziwa na kampuni hizo.

Kampuni zinazolalamikiwa na wafanyabiashara hao wa mafuta ni Gapco ambayo baadaye ilinunuliwa na Total.

Mmoja wa wauzaji wa mafuta wa jijini Dar es Salaam, ambaye hakupenda jina lake litajwe gazetini alisema kampuni hizo zimekuwa zikitoza kuanzia Sh. 22 hadi 67 kwa kila lita ya mafuta wanayowauzia.

"Kila mwezi Ewura wanatoa bei elekezi sasa kwa mfano wakitoa bei elekezi iwe Sh. 105 kwa lita ya petroli wao wanatukata kuanzia Sh. 22 hadi 67 kwa kila lita jambo ambalo ni kinyume kabisa na taratibu na ndiyo sababu unakuta mafuta yako juu ," alisema mfanyabiashara huyo.

Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Maji na Nishati (EWURA), Titus Kaguo, alikiri kupokea malalamiko ya wafanyabiashara hao na kwamba tayari walishaziandikia barua za onyo kampuni za Total na Gapco.

"Hao wafanyabiashara walishafikisha malalamiko yao kwetu na tukaona ni malalamiko ya haki kabisa kwa sababu hayo makato wanayowakata si halali kikanuni tumewaandikia wasitishe makato hayo," alisema Kaguo. Aidha, Kaguo alisema baada ya kuwaandikia, wenye kampuni hizo waliwajibu kwamba watakutana na wafanyabiashara hao ili wayamalize lakini bado hawajarudi EWURA kusema kama kweli wameyamaliza.

Mfanyabiashara mwingine wa mafuta mkoani Morogoro ambaye naye hakutaka atajwe alisema kwa kawaida wenye kampuni kubwa za mafuta wanajenga vituo na kuwapa wafanyabiashara wazalendo kuviendesha.

Alisema sharti la kuendesha vituo hivyo vya mafuta ni kununua mafuta yote kwenye kampuni hizo zilizojenga kituo cha mafuta lakini wameshangaa kuona makato hayo.

"Sisi tunanunua mafuta kutoka kwao hawatupi bure ila tunatumia vituo walivyojenga wao kufanya biashara hii sasa makato hata Ewura haiyatambui ni kiburi tu cha hizi kampuni kubwa," alisema mfanyabiashara mwingine wa mafuta.

Alisema kuna kampuni zingine za kimataifa kama Puma, Engine, Oryx na Kobil ambazo zimekuwa zikijenga vituo vya mafuta na kuwapa wafanyabiashara wadogo waviendeshe, hazina makato ya aina hiyo. Alisema mafuta yanayoingia nchini yanalipiwa kodi zote isipokuwa ile ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo kampuni hizi kubwa zinawakata wafanyabiashara hao kwenye bei elekezi inayotolewa na Ewura wanapaswa kulipa kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Alisema awali kampuni hizo zilikuwa zikiingiza makato hayo kwenye bei wanayokuuzia mafuta lakini baada ya wao kulalamika Ewura na kuonywa wakabadili mtindo na kuanza kuwapelekea hati mbili za malipo (invoice).

Mkurugenzi wa Habari na Elimu kwa Umma wa TRA, Richard Kayombo alipoulizwa iwapo kuna kodi yoyote ambayo wanakwepa wafanyabiashara hao alisema mamlaka hiyo hukata kodi yake mafuta yanapoingia nchini tu.

"Sisi tunakata kodi yetu mapema tu mara mafuta yanapoingia nchini sasa kama hao wanalalamika watakuwa wanalalamikia tozo zingine na siyo kodi na watu sahihi hapo wa kuwaona ni Ewura watakufafanulia kuhusu hizo tozo zingine," alisema Kayombo.

Nipashe ilifika kwenye ofisi za kampuni hiyo Masaki jijini Dar es Salaam ili kupata maelezo ya upande wa pili lakini mwanasheria wa kampuni hiyo aliyefahamika kwa jina la Masha alisema hakuwa na muda wa kuonana na mwandishi wakati huo.

## Chuo kuboreshwa kuongeza ubunifu

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii na Wizara ya Viwanda na Biashara inakusudia kuwekeza katika kituo cha ubunifu kilichoko katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mabughai, Tanga ili kukiwezesha kutoa elimu yenye tija kwa wahitimu na jamii kwa ujumla.

Hayo yamebainika wakati wa ziara ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alipotembelea chuo hicho kujionea shughuli zinazofanywa na chuo hicho.

Dk. John Jingu alisema amefanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, ili kukiwezesha chuo kutoa mafunzo ya ubunifu endelevu kwa jamii.

Alisema mpango wa maboresho ya miundombinu na teknolojia ya chuo hicho utashirikisha Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na chuo kilicho chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Teknolojia imebadilika sana mimi na Profesa Shemdoe tumekubaliana kufanya maboresho katika chuo hiki tuone namna ya kukiwezesha kuwanoa wabunifu, ili elimu inayotolewa kuwa na tija kwa walengwa wetu ambao ni wanachuo na wananchi wa maeneo jirani," alisema.

Alisisitiza kuwa serikali inalenga kuwawezesha wanafunzi kuwa na uwezo wa kujiajiri kupitia maarifa wanayopata na kuanzisha mtandao wa ajira kwa wahitimu ambao watafanya kazi kwa vitendo, hivyo kutengeneza fursa zaidi za mafunzo kwa wengine.

Katibu Mkuu Jingu alisema mpango wa kuboresha chuo hicho utaanza hivi karibuni baada ya kukamilisha taratibu za maandalizi kwa ushirikiano wa SIDO na ni hatua mojawapo ya kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda. "Tumeshuhudia jitihada za serikali zilivyotuwezesha kuingia katika uchumi wa kati miaka mitano kabla ya muda uliotarajiwa wakati tukiendelea kujivunia hatua hii muhimu kushiriki kwa vitendo katika mabadiliko ya teknolojia," alisema.

"Kuna baadhi ya mafanikio yaliyopatikana hadi sasa. Mfano kuna mbunifu ametoa ajira kwa zaidi ya watu 100. Hii ni hatua mojawapo ya mafanikio. Tunataka kukiwezesha chuo hiki kutengeneza wabunifu zaidi," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Binilith Mahenge (kulia) na Msimamizi Mkuu wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) mkoa huo, akikagua majina ya wajumbe, kabla ya kupiga kura ya maoni ya kuwachagua wabunge wa viti maalum kwenye makundi matano ya NGO, wasomi, walemavu, wafanyakazi na UWT, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# NEC yaonya watendaji wake kupendelea vyama uchaguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, amewataka wasimazi wa uchaguzi nchini kutotekeleza majukumu yao kwa kuegemea upande mmoja au kujihusisha na chama chochote.

Pia, amewataka wasimamizi hao kuzingatia Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sheria ya Uchaguzi pamoja na melekezo yanayotolewa na NEC na siyo vinginevyo.

Jaji Kaijage alitoa maagizo hayo jana jijini Dodoma alipofungua kikao kazi cha wasimamizi wa uchaguzi Tanzania Bara kwa ngazi ya urais, ubunge na udiwani unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Alisema wasimamizi wa uchaguzi wanatakiwa kujitambua na kuacha kutekeleza majukumu yao kwa kuonyesha kuwa wameegemea upande fulani au kujihusisha na upande wowote wa uchaguzi.

"Wasimamizi wa uchaguzi lazima tujitambue, tusitekeleze majukumu yetu kwa kuonyesha tumeegemea wapi au kujihusisha na upande wowote wa uchaguzi," aliagiza.

Jaji Kaijage alisema uchaguzi mkuu unaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu, hivyo wasimamizi wanatakiwa kuzingatia maelekezo na siyo kufanya kazi kwa matakwa yao.

"Wasimamizi wanatakiwa kuzingatia sheria za uchaguzi kwani kwa kosa lolote atakalofanya, anaweza kuingia katika jinai, hivyo ni vyema kila mmoja akazingatia maelekezo na kufuta sheria katika kusimamia uchaguzi mkuu," alionya.

Vilevile, Jaji Kaijage aliwataka wasimamizi hao kuanza kuandaa mipango ya uchaguzi mapema, ili kubaini dosari ambazo zinaweza kuharibu mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Tumeona ni vyema tukapeana mambo ambayo tunatakiwa kuyazingatia kuelekea uchaguzi mkuu ili kuepuka dosari zinazoweza kuharibu uchaguzi mkuu.

"Pia, wasimamizi wa uchaguzi mnao wajibu wa kufanikisha uchaguzi mkuu kwa kuandaa mipango ya uchaguzi na kubaini maeneo yanayoweza kuharibu uchaguzi, ili kuyafanyia kazi mapema," alisema Jaji Kaijage.

Aliwataka wasimamizi wa uchaguzi wote kuhakikisha wanakuwapo katika vituo vyao vya kazi katika kipindi chote cha uchaguzi ili kuepusha malalamiko yasiyo ya lazima.

Akizungumzia kuhusu uboreshaji wa daftari la wapigakura, Jaji Kaijage alisema kwa awamu mbili za uboreshaji, jumla ya wapigakura wapya 7,326,552 wameandikishwa, sawa na asilimia 31.63 ya wapigakura 23,161,440 walioandikishwa mwaka 2015.

"Jumla ya wapigakura 30,487 waliondolewa kwenye daftari la kudumu la wapigakura kutokana na kukosa sifa kwa mujibu wa sheria. Baada ya kutoa wapigakura ambao taarifa zao zimejirudia, taarifa za awali zinaonyesha kuwa daftari lina jumla ya wapigakura takribani milioni 29," alibainisha.

Mkurugenzi wa Uchaguzi, Dk. Wilson Charles, alisema kikao kazi hicho kimehusisha wakurugenzi wote ambao ndiyo watakuwa wanawajibika moja kwa moja kwa tume hiyo.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu unafanyika bila kuwapo kwa malalamiko, hivyo wasimamizi wote wanatakiwa kuzingatia mafunzo yatakayotolewa katika kikao hicho, ili wakawasaidie walioko chini yao.

# 'Msidhalilishe wagombea wa uchaguzi mkuu 2020'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISA Uchechemuzi Habari na Mawasiliano wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), amewataka waandishi wa habari nchini kuripoti habari za uchaguzi mkuu kwa kuzingatia misingi na kanuni za uandishi wa habari, ikiwamo kutowadhalilisha wagombea hasa wanawake.

Florence Majani, alitoa rai hiyo alipofungua mafunzo ya waandishi wa habari kutoka mikoa ya Arusha na Dodoma, yanayolenga kuwajengea uwezo wa namna ya kuripoti vyema habari za jinsia wakati wa uchaguzi mkuu mwaka huu. Majani alisema wanawake wengi wamejitokeza kugombea nafasi mbalimbali, hivyo ni wajibu wa waandishi wa habari kuandika habari ambazo haziwadhalilishi, ili kuleta usawa wa kijinsia. Alisisitiza waandishi kutoa elimu kwa wanawake ili wasitoe wala kupokea rushwa katika michakato ya uchaguzi.

"Kipindi hiki wanawake mnapaswa kutoa taarifa za uwapo wa mazingira ya rushwa, ili kusaidia kupata viongozi wenye sifa zinazohitajika," alisema.

Mwezeshaji katika mafunzo hayo ambaye pia ni Wakili na Mwanachama wa TAMWA, Marry Mwita, alisema kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, kila mwananchi ana haki sawa na wengine na kuwataka waandishi wa habari kutofumbia macho vitendo vya ukandamizaji wanawake.

Alisema wanawake wana haki ya kuchaguliwa bila kutoa rushwa, akifafanua: "Waandishi mnapaswa kuzisema changamoto hizi ambazo zinatokea kwenye kipindi cha uchaguzi, ili zifanyiwe kazi, na wanawake wengi wachaguliwe kwa sifa zao kwa kuwa wana uwezo wa kuongoza."

# TCRA sasa yapata dawa mashambulizi mtandaoni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mawasiliano (TCRA), imeunda chombo cha kudhibiti mashambulizi ya kimtandao nchini kwa kushirikiana na vyombo vingine vya nje ya nchi.

Mkurugenzi wa Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa TCRA, Connie Fransis, alibainisha kuundwa kwa chombo alipofungua semina ya wiki mbili ya udhibiti usalama wa kimtandao na namna ya kukinga mifumo kwa kuifanya iwe imara, ili isiingiliwe kwa urahisi.

Alisema udhaifu wa mifumo ya kimtandao ndiyo unaosababisha mashambulizi ya njia ya kimtandao kwenye taasisi za umma na binafsi.

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na utengenezwaji wa mifumo, kumekuwa na upungufu ambapo huwezesha mfumo kuingiliwa na kufanyiwa mashambulizi na kwamba kitendo hicho huwa ni cha dakika chache.


Connie alisema kuna haja wataalamu hao kuhakikisha wanachunguza mifumo yao mara kwa mara na kuangalia upungufu uliopo kwa kujua mifumo yao kwa undani ili kudhibiti mashambulio hayo ya kimtandao.

"Kitengo hiki ndani ya TCRA kazi yetu kubwa ni kuisaidia serikali kwa kuhakikisha mifumo ya taasisi inakuwa imara, tunashirikiana vyema na nchi ya Uganda, Tanzania, Rwanda na Kenya katika udhibiti huo maana matukio ya mashambulizi yanafanana kutokana na aina moja ya mifumo inayotumika," alisema.

Alisema jukumu lingine la kitengo hicho ni kuhakikisha taasisi za serikali zinaingia kwenye mfumo wa kanzidata, maana wakiwa nje ya mifumo wanapopata tatizo, inakuwa vigumu kulitatua.

Mkurugenzi huyo alisema wamekuwa wakifanya mafunzo hayo mara kwa mara kwa wataalamu hao kwa lengo la kuwajengea uwezo na kuwawezesha kuimarisha mifumo yao maana vita ya mtandao inazidi kuwa kubwa.

Aliwataka kujifunza zaidi na zaidi ili wawe na uelewa mpana na kutoa elimu kwa wengine ambao hawajapata nafasi ya mafunzo.



# Majina makubwa yaangushwa kura za maoni ACT-Wazalendo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ALIYEKUWA Mbunge wa Malindi kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Ali Abdallah Saleh, ameangushwa katika kura za maoni za kuwania nafasi hiyo kupitia ACT- Wazalendo.

Saleh ni miongoni mwa waliokuwa wabunge na wawakilishi waliojitosa kutetea nafasi hiyo kupitia chama hicho baada ya kuvihama vyama vyao walivyokuwa wakitumikia nafasi hizo.

Katika uchaguzi huo wa kura za maoni, Saleh alipata kura 20 dhidi ya Mohamed Ibrahim Sanya aliyepata kura 56. Halima Ibrahim Mohamed alishika nafasi ya pili kwa kupata kura 36.

Kwa nafasi ya uwakilishi katika jimbo hilo, Ismail Jussa Ladhu aliongoza kwa kupata kura 90 akifuatiwa na Hussein Keisy aliyepata kura 29. Jimbo la Donge, aliyeshinda uwakilishi ni Pavu Juma Abdallah aliyepata kura 57 na hakuwa na mpinzani wakati nafasi ya ubunge, aliyeongoza ni Hussein Kassim Sheha kwa kupata kura 59 za ndiyo kutokana na kutokuwa na mpinzani. Jimbo la Mahonda, aliyeongoza nafasi ya uwakilishi ni Thuwaiba Juma Hussein aliyepata kura 37 na ubunge ni Sauda Makame Khatib aliyejizolea kura 38. Katika Jimbo la Bumbwini, Uwakilishi ni Zahran Juma Mshamba aliyepata kura 181. Na ubunge ni Mohamed Amour Mohamed aliyeshinda kwa kura 101 huku Micheweni Haji Khatib Kai akiongoza kura za maoni za ubunge kwa kura 107 na uwakilishi akiongoza Mbarouk Omar Abdalla aliyepata kura 53.

Konde, aliyeshinda ubunge ni Khatib Said Haji aliyepata kura 232 akimshinda Juma Hamad Khalid aliyepata kura 97. Aliongoza katika uwakilishi ni Issa Said Juma aliyepata kura 148.

Katika kinyang'anyiro cha ubunge Jimbo la Wingwi, Kombo Mwinyi Shehe aliongoza kwa kupata kura 88 na uwakilishi ni Juma Kombo Hamad aliyepata kura 104. Jimbo la Mfenesini, nafasi ya uwakilishi ni Suleiman Mohamed Bakari, Jimbo la Magomeni ni Haji Dude Haji, Mpendae ni Ali Hamad na Jimbo la Uzini ni Amran Naima. Aliyeongoza Jimbo la Makunduchi ni Azizi Mohamed Ali na Jimbo la Pangawe ni Suleiman Simai Pandu.




Mkuu wa Biashara wa Zantel, Aneth Muga, akizungumza na waandishi wa habari Zanzibar juzi, wakati wa uzinduzi wa huduma mpya maarufu kama 'Bando Halikati', inayowawezesha wateja kuvusha dakika na MB za intaneti za mtandao huo, kutoka kifurushi cha awali kwenda kifurushi kipya. Kushoto ni Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohamed Khamis Mussa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waathirika ukatili wapewa msaada

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

FAMILIA za waathirika wa udhalilishaji kisiwani Pemba, wameshukuru na kupongeza juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar za kupambana na vitendo hivyo katika jamii.

Pongezi hizo zilitolewa jana kwa nyakati tofauti na baadhi ya wanafamilia hao baada ya kukabidhiwa kuku kwa ajili ya ufugaji ikiwa

ni sehemu ya juhudi za chama hicho kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

Mmoja wa wanufaika wa msaada huo, Mpemba Ali Mohamed alisema kuku hao watawasaidia kujiendeleza kiuchumi kulingana na hali ngumu ya maisha wanayokabiliana nayo.

"Tunawashukuru sana TAMWA kwa kutambua matatizo yetu na kuamua kutuletea msaada huu kama sehemu ya faraja kwetu. Tunajisikia furaha sana kwa kweli leo (juzi)," alisema.

Pia aliongeza kuwa kutokana na familia hizo kuwa katika hali ngumu ya maisha, kupitia ufugaji wa kuku watakuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma za msingi katika familia zao.

"Kupitia kuku hawa tuliopewa leo (juzi) watatusaidia sana kutatulia shida nyingi kama vile chakula kulingana na hali zetu ndiyo kama hivyo hatujiwezi na hatuna shughuli nyingine yoyote ya kutupatia kipato," alisema Mpemba.

Naye Shaali Makame Sahaali alisema licha ya kuku hao kuwasaidia kujiendeleza kiuchumi, pia misaada hiyo imechochea hamasa kwa familia hizo kujiona kuwa sehemu ya jamii.

"Niseme tu kwamba TAMWA imefanya jambo kubwa sana kwani licha ya mitihani tuliyokumbana nayo, kupitia hili na sisi tumefarijika sana na kujiona kuwa sehemu ya jamii," alisema.

Akizungumza wakati wa utoaji misaada hiyo, Katibu wa Sheha ya Kiwani, Wilaya ya Mkoani Pemba, Mohamed Haji Suleiman, alishukuru mchango wa TAMWA Zanzibar katika kulinda na kutetea haki za kijamii na kukitaka chama hicho kuendelea na juhudi hizo ili kuhakikisha jamii inabaki salama.

"Juhudi hizi zinazoendelea kuchukuliwa na TAMWA si kazi ndogo. Niwaombe sana endeleeni na juhudi hizi ili kuhakikisha mnasaidia kutokomeza vitendo vyote vya udhalilishaji katika jamii zetu Zanzibar," alisema.

Mratibu wa TAMWA Zanzibar Ofisi ya Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema lengo la kutoa msaada wa kuku kwa familia za waathirika hao ni kuwawezesha kuwa na shughuli za kujiingiza kipato katika familia.

"Tumeamua kutoa msaada huu kwa familia hizi ili uwasaidie kuendesha familia zao kutokana na wengi wao kuwa katika hali ngumu ya maisha," alisema.

Alisema hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa kupinga udhalilishaji Zanzibar katika kuwawezesha waathirika kujihusisha na uzalishaji ili kuwa na uwezo wa kufuatilia kesi zao mahakamani.

Kuku 300 wamegawiwa kwa familia 30 za waathirika wa vitendo hivyo kutoka Wilaya za Mkoani na Wete Pemba.

## Zanzibar yaishukuru WHO mapambano dhidi ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya wa Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed, amelishukuru Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa juhudi kubwa katika kushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mapambano dhidi ya maradhi ya corona nchini.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake, Mnazi Mmoja mjini hapa wakati akizungumza na Mwakilishi wa WHO, Dk. Andemichael Ghirmy, aliyefika kujua hatua iliyofikia kwa maradhi hayo.

Hamad alisema kwa sasa maradhi hayo yamedhibitiwa kwa kiasi kikubwa hali ambayo imewapa matumaini ya kuruhusu shughuli za kazi kuendelea kama kawaida na kuruhusu wageni, wakiwamo watalii, kuingia bila pingamizi.

"Tumeruhusu wageni waingie nchini bila wasiwasi wowote kwani tumejipanga vizuri kwa matibabu na kuwashughulikia kwa kuwapima na kujua taarifa zao kwani Zanzibar maradhi haya yamepungua kwa kiasi kikubwa. Ikigundulika na mmoja wao ana maradhi, tutahakikisha tunampatia matibabu ipasavyo," alisema Hamad.

Aidha, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalipongeza shirika hilo kwa kuwa mafanikio hayo yametokana na juhudi ya pamoja kwa kutoa misaada yao na kupeana taarifa za kitaalamu.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa wageni wanaoingia kwani bado zipo nchi za jirani zinasumbuliwa na maradhi hayo.

Aliwataka washirika wa maendeleo kuendelea kuwaunga mkono inapotokea mlipuko wa maradhi ya aina yoyote yakiwamo kipindupindu na malaria ili kuyadhibiti kwa haraka sana.

Naye Dk. Ghirmy alisema ataendelea kushirikiana na serikali kupitia Wizara ya Afya na kuhakikisha wanakwenda sambamba na maradhi ya mlipuko ambayo yanaweza kujitokeza.

Alisema licha kupungua kwa maambukizi ya corona nchini, pia wanajipanga kutokomeza kipindupindu Zanzibar kupitia Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa ili kuhakikisha maradhi hayo yanaondoka kabisa kwa Unguja na Pemba.



PROFESA JAY

UKURASA 12







# OLE WENU VIHEREHERE

# Mzee Yusuf karudi tenaaaa

HATIMAYE ni rasmi Mfalme wa Taarab nchini, Mzee Yusuf, anarudi tena baada ya kukaa nje ya muziki huo kwa miaka mitano.

Msanii huyo aliyepata umaarufu kutokana na umahiri wake wa kuimba taarab, aliamua kutangaza kuacha muziki na kasha kuegemea kueneza imani ya dini yake ya Kiislamu.

Katika muda huo, Mzee Yusuf, alijihusisha na uimbaji wa nyimbo za Qasida ambazo zilipendwa na waumini wa dini hiyo.

Hata hivyo, wiki hii Mzee Yusufu, alitangaza kurudi tena katika muziki wa Taarab na kupanga siku ya tarehe 31, itakuwa maalum kwa ajili ya kujitambulisha.

Hata hivyo, amesema hawezi kusema sababu za kurudi tena, lakini amekaa na kutafakari kwa kina kabla ya kuamua kuchukua hatua hiyo.

"Miaka mitano sijaimba taarabu, sijakuwa na sababu ya kufanya hivyo na hata ninaporudi siwezi kusema kitu chochote," amesema.

Hata hivyo, amewasihi watu wasiwe na jazba kutokana na hatua yake hiyo, bali watambue adhabu zote zitabaki kuwa kwake.

"Sina jinsi, madamu sijaacha dini yangu, wale watakaopandwa hasira watambue huu ni uamuzi wangu, watu hawana mamlaka ya kunihukumu, Mungu ameshapanga adhabu yake toka zamani," amesema.

Ameongeza kwamba maisha ndani ya miaka hiyo mitano ilikuwa na magumu mengi kiasi ambacho mali zake zimewekwa mnadani na hakuna mtu aliyejitokeza kumsaidia.

"Nilikaa nikaona hiki kimefeli, kile kimefeli hapo nikaanza kufikiria sana, hakuna mtu aliyenisaidia nataka mtu atokee aanze kusema maneno mimi nitajibu, akisema kwenye TV nitamjibu kwenye radio," ameongeza kusema.

BASI SAWA

## Profesa Jay kama mwanafalsafa wa kale

RAPA na Mbunge wa Mikumi, Profesa Jay, amesema katika maisha yake amejifunza kwamba kuchunga mdomo ni jambo muhimu.

Katika ujumbe alioweka katika ukurasa wake wa Instagram, Jay ameandika kuwa, kila baya unalofanya duniani malipo yake utayapata hapahapa na hakuna kusubiri.

"Nimejifunza kwamba sisi wanadamu inatupasa kuchunga sana ndimi zetu, kutafakari kwa kina kauli zetu na inapobidi ni kufunga kabisa mabakuli yetu kwani malipo yapo hapa hapa duniani na mwisho wa ubaya ni aibu," ameandika Jay.



## Idris usimcheke mwenzio, yatakukuta na wewe

MWIGIZAJI na mchekeshaji, Idris Sultan, amejifariji kwa kitendo cha msanii mwenzake Steve Nyerere, kuanguka katika kura za maoni za CCM, akisema hata yeye alimwongelea mbovu kwenye mahojiano aliyofanya hivi karibuni.

Steve alishindwa kwenye kura za maoni ya kuwania ubunge wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kupata kura tano.

"Sitaki kuwa mnafki, kaka Steve juzi kaniongelea mbovu sana kwenye mahojiano, mambo ambayo hata kama ni kweli au la angeweza niambia mwenyewe, nikahojiwa na mimi nikasema siweziongea ni mkubwa wangu tena hasa sasa anavyoutafuta ugali wa chama, Mungu awe nawe kwenye wakati huu mgumu," ameandika Sultan kwenye Twitter.





## Mjomba Fujo afyatua kibao kumsifu 'Anko Magu'

MSANII wa muziki wa kizazi kipya nchini, George Paul, maarufu kama 'Mjomba Fujo' anakuja na kazi mpya ambayo ni maalum kwa ajili ya kupongeza utendaji wa Rais John Magufuli.

Huu ni wimbo wa pili kwa msanii huyo, ambapo awali aliachia hewani wimbo aliupa jina la 'Huyu ndiye Magufuli, mtetezi wa Wanyonge'.

Akizungumzia kazi yake hiyo mpya, Mjomba Fujo amesema, kilichomo ndani ya wimbo huo ni kupongeza kila hatua aliyoifanya Rais Magufuli kwa kuwatumikia watanzania, hivyo anaomba Watanzania waendelea kumwamini tena katika awamu ijayo.

Alisema, anaamini hayo kwasababu kila nyanja ambazo ni muhimu kwa ajili ya maisha ya kila siku ya Watanzania ameyagusa kwa ufanisi, hivyo anaomba wapiga kura kumpa nafasi tena ya kumalizia pale alipoishi.

"Ni wimbo ambao ujumbe wake uko wazi kwamba ni kiongozi aliyeonyesha dhahiri kuwa anapambana kwa ajili ya kuona Tanzania inapiga hatua na kutatua kila kero, jambo ambalo amefanikiwa kwa asilimia kubwa, hivyo anafaa aendelee kupewa dhamana hii," amesema Mjomba Fujo.

## Sijapoteza: Thamani ya mkia hadi ukatwe

**Na Adam Fungamwaango**

UPO msemo wa Kiswahili kuwa mbuzi hajui thamani ya mkia wake hadi ukatwe.

Maana ya msemo huu ni kwamba wakati mwingine binadamu hawezi kuona umuhimu au thamani ya kitu alichonacho, hadi kipotee, anyang'anywe au kiishe, ndipo anapotambua kuwa alichokuwa akikimiliki kilikuwa na umuhimu.

Nyimbo nyingi za zamani na za sasa zimetungwa na kuimbwa kuhusiana na jambo hili. Hata filamu zimeshatungwa sana. Moja wapo ni hii iitwayo 'Sijapoteza'.

Imechezwa na wasanii Amri Athumani, maarufu kama mzee Majuto (marehemu), Mboto, na Getrude Mwakabana.

Filamu inaanza kuonyesha kuwa Mboto na mkewe Salma, wanaishi kwa amani, wakiwa na mzee wao mzee Majuto ambaye ni baba wa Mboto.

Hata hivyo, tabia ya Mboto na baba yake mzazi haziridhishi. Mboto ana tabia ya kupenda wanawake ovyo. Amekuwa akibadilisha mademu anavyopenda. Halafu ni mtu ambaye hana hata heshima kwa mkewe, kwani kuna wakati hata mke amekuwa mara kwa mara anamfuma na wanawake.

Waswahili wanasema mtoto wa nyoka ni nyoka, inawezekana kabisa kuwa tabia hii amerithi kutoka kwa baba yake, kwani mzee Majuto amekuwa na tabia hiyo hiyo.

Pamoja na utu uzima wake, amekuwa wakitongoza wasichana wadogo ambao kiumri ni sawa na wajukuu zake.

Mashtaka na mlalamiko yakawa hayakauki nyumbani kwao, lakini baba na mtoto wote akili zao ni sawa.

Salma ambaye alikuwa anajitahidi kusuluhisha, kuomba radhi, lakini na yeye mwenyewe akawa anakumbana na mambo kama hayo.

Kuna wakati baba na mwanawe wanatoka usiku kwenda kwenye vigodoro, kwa sababu tu eti ya kuangalia mademu wakali.

Baba wa mwanamke akawa mara kwa mara anakuja nyumbani na kumtaka binti yake aachane na mwanaume huyo, lakini Salma alimpenda sana Mboto, ila tu mwanaume akili zake alikuwa anazijua mwenyewe na baba yake mzee Majuto.

Mzee Majuto akatokea kumpenda rafiki wa mkwewe na kutaka eti afanyiwe mipango, lakini kwa kumkomoa wakajifanya wamekubali.

Kilichofanyika ni kutafuta vijana ili wajifanye kama wanamfumania na kumpiga kidogo kwa ajili ya kumshikisha adabu, aachane na mambo hayo. Na ndicho kilichofanyika. Mzee Majuto tangu siku hiyo akajirekebisha.

Mambo yalizidi kuwa mabaya kwa Salma, akasalimu amri na kuamua kuondoka nyumbani.

Siku tatu tu tangu aondoke, tabu ikaanza. Kula ikawa tabu, Mboto akaona kabisa nyumbani kuna vitu vinapungua.

Wakafanya mipango kwenda kuvamia nyumbani kwa baba wa Salma ili wamteke, lakini mzee akawatokea na bastola, wakakimbia.

Ikabaki sasa kilio na kusaga meno. Mboto na mzee Majuto kila mtu akawa anamlaumu mwenzake kutokana na tabia mbaya.

Mboto akaamua aondoka hapo aende sehemu yoyote kuanza maisha mapya, kwani aliona mpweke.

Katika hali isiyotarajia, mlango unafunguliwa na Salma anaingia. Wote wanashangaa. Anawaambia amerejea, kwani amewakumbuka na anampenda sana Mboto, ila ajirekebishe. Mboto anaomba radhi.








## H Baba kawa chawa wa Harmonize?

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, H-Baba, ameamua kuwatolea uvivu watu wanaosema kuhusu urafiki wake na Harmonize, akisema wacha waseme lakini hawezi kuvunja ukaribu wao.

Akizungumza na EATV, H Baba, amesema ataendelea kuwa chawa wa Harmonize kama wanavyosema watu mitandaoni, ila atasimama imara kwani hata Harmonize amemkuta hivyo hivyo.

"Ni vizuri sana kwani ni maoni ya watu hutakiwi kuyapinga, mimi ni shabiki namba moja wa Harmonize pili ananiheshimu, acha niwe chawa wa Harmonize kama wao wanavyojua ila mimi nasimama kama H Baba kwa sababu hata Harmonize amenikuta nikiwa hivi, " ameeleza H-Baba.

## Wasanii waliojaribu, wakaangukia pua

**Na Adam Fungamwango**

HIVI karibuni kuliibuka na kundi la mastaa mbalimbali kuchangamkia fomu za kupitishwa kugombea ubunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wengi walikwenda kuchukua fomu, labda wakidhani kutokana na umaarufu wao ingekuwa rahisi kwao kupita kwenye kura za maoni, lakini ikawa kinyume chake.

Wajumbe wa CCM, walitumia haki na demokrasia yao kuchngua ni nani wanaowapendeleza ili kwenda kupeperusha bendera ya CCM kuwania ubunge kwa tiketi hiyo.

Labda wengi wakaona kama wakiwapeleka bungeni, huku kwingine watakosa uhondo na wanatakiwa wakae kwenye nafasi zao ili waendelee kupata burudani. Wasanii wabaki kuwaburudisha na wanasiasa kuwaongoza.

Huu msemo ndiyo uliotumiwa na wajumbe wa CCM Tanzania nzima na kuwafanya mastaa wengi kuanguka, huku wachache tu ndiyo wakipita.

Hawa ni baadhi ya mastaa ambao walichukua fomu kugombea kuteuliwa kuipeperusha bendera ya CCM kwenye uchaguzi utakaofanyika mwezi Oktoba.

**Mpoki**

Huyu anajulikana kama msanii na vichekesho. Kwa sasa pia amekuwa ni MC kwenye sherehe mbalimbali za kijamii au taasisi mbalimbali. Jina lake kamili ni Silvery Mjuni. Alichukua fomu kutaka kupitishwa na CCM kugombea ubunge kwenye Jimbo la Kigamboni. Kwa bahati mbaya sana hakuambulia hata kura moja.

**Steve Nyerere**

Ni mwigizaji wa filamu za Bongo Movie, lakini ni msanii na mwigizaji za filamu za vichekesho.

Alama yake kubwa ni kuigiza sauti ya Baba wa Taifa, marehemu Mwalimu Nyerere na ndiyo iliyompatia sana umaarufu, mpaka mwenyewe kujiita Steve Nyerere. Jina lake halisi ni Steven Mengele. Alichukua fomu kutaka kupitishwa kuipeperusha bendera ya CCM kupitia Iringa Mjini.

Kilichotokea ni kwamba aliambulia kura sita tu.

**MC Pilipili**

Jina lake halisi ni Emmanuel Mathias. Yeye alitangaza nia ya kutaka kuiwakilisha CCM kwenye uchaguzi mkuu, akichukua fomu kwenye Jimbo la Bahi kwenye Jiji la Dodoma.

Naye pia kwa bahati mbaya sana alitoka mikono mitupu. Maana yake ni kwamba hakuambulia hata kura moja.

**Zamaradi Mketema**

Ni mmoja kati ya mastaa wakubwa nchini Tanzania. Ni mtangazaji ambaye amejizolea umaarufu mkubwa nchini. Alitia nia kwenye Jimbo la Kinondoni, moja kati ya majimbo magumu mno nchini Tanzania. Wenyewe wanasema ndiyo jimbo la watoto wa mjini. Yaani wenyewe wanasema Dar es Salaam ni Kinondoni. Mketema aliambulia kura mbili tu.

**Kalapina**

Wengi wanamkumbuka msanii huyu kama mwimbaji wa hip hop kutoka kikosi cha mizinga. Jina lake kamili ni Karama Masoud. Alichukua fomu kugombea kupitishwa kuiwakilisha CCM kupitia jimbo la watoto wa mjini, Kinondoni.

Kalapina ambaye yeye pia ni mtoto wa mjini, mtoto wa Kinondoni, lakini hiyo haikumfanya kushinda, badala yake akaambulia kura moja tu.

**Master Jay**

Joachim Marunda Kimaryo alichukua fomu kwa ajili ya kutaka kupitishwa na CCM kugombea kwa tiketi hiyo, kwenye Jimbo la Rombo. Huyu ni mtayarishaji mkongwe wa muziki nchini Tanzania.

Jina lake maarufu ni Master Jay. Yeye alinyoa kabisa rasta zake, ili kujiandaa kuwa mheshimiwa.

Hata hivyo, aliambulia kura mbili tu kwenye kinyang'anyiro hicho.






# Kanye hukosagi vituko

RAPA maarufu Kanye West ameibua mazito baada ya kudaiwa kutaka kuivunja ndoa yake kwa kumpa talaka mkewe Kim Kardashian.

Mwanamuziki huyo ambaye amepanga kuwania urais wa Marekani mwaka huu, alitoa madai hayo katika ukurasa wake wa Twitter, akisema alichanganyikiwa wakati akifikiria jambo hilo.

Kulingana na ujumbe wake, West alitaka kuchukua hatua hiyo baada ya Kim kuonekana akiwa na msanii mwenzake wa Hip hop, Meek Mill.

West na Mill wapo katika bifu kali kwa muda mrefu na hakuna dalili ya kupatana.



## Piga makofi! Minaj mama kijacho

MWANAMUZIKI nyota wa Hiphop nchini Marekani, Nicki Minaj, amewashangaza mashabiki wake baada ya kuonyesha hadharani ujauzito wake.

Picha za rapa huyo akiwa na tumbo kubwa zilisambaa kwenye mitandao, huku mashabiki wake wakigawanyika kwa kueleza kuna uwezekano mkubwa Minaj amejifungua.

Katika picha hiyo, Minaj alionekana akiwa na tumbo linaloashiria miezi ya kujifungua imekaribia, hivyo kuongeza nguvu ya viashiria kwamba mwanamuziki huyo tayari amepata mtoto wake wa kwanza.

## Wizkid hujui mtoto wa nyoka ni...

MKALI wa muziki kutoka Nigeria, Ayo Balogun, maarufu kama Wizkid, ameonyesha kipaji cha muziki cha mtoto wake wa kiume.

Wizkid ameonekana akiwa na mtoto wake huyo Zion ndani ya studio ya muziki, huku mwanawe akijaribu kuchezea baadhi ya vifaa.

Picha hiyo ambayo imepostiwa na mama yake Jada, ilionekana kupendwa na mashabiki wengi waliofuatilia katika akaunti ya Instagram ya mwanamuziki huyo.





## Demi hongera kuvishwa pete

MWANAMUZIKI wa Marekani, Demi Lovato, hatimaye amevishwa pete na mchumba wake ambaye ni mwigizaji Max Ehrich.

Nyota huyo mdogo ametumia ukurasa wake wa Instagram, kuonyesha hadharani pete hiyo ambayo ni ya gharama kubwa.

"Kwangu imenifanya niwe na hakika, na leo maneno yamegeuka kuwa dhahiri tena, lakini sasa ni maalum nakuwa na mwenza wangu," ameandika Demi.

## Yusuf tangulia tuko nyuma yako

MWIGIZAJI kutoka jamii ya Yoruba, Yusuf Satia, ameaga dunia.

Nyota huyo wa filamu za Nollywood, alianza kufahamika tangu mwaka 2000 baada ya kutoka na kazi yake inayoitwa Injile Pam Pam.

Kulingana na rafiki wake wa karibu, Kunle Afod, aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kwamba sekta ya filamu imepata pigo lingine baada ya mkongwe huyo kufariki dunia juzi.



MAKALA

# Mimba mabinti sekondari za Iramba 'pasua kichwa'

## ■ Likizo ya corona na majanga yake

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa** IRAMBA



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya New Kiomboi wiayani Iramba, mkoani Singida. **PICHA: MTANDAO**

SHULE zimeshafunguliwa ni wastani wa mwezi mmoja sasa. Katika shule za sekondari za Halmashauri ya Manispaa ya Iramba mkoani Singida kuna yake.

Katika Shule ya Kizaga iliyoko kilomita moja na nusu kutoka barabara kuu ya magari makubwa yaendayo mikoa mbalimbali. Ina jumla ya wanafunzi 706, kati yao wasichana 391 na wavulana 316.

Kuna wasichana 80 wanaoishi katika hosteli yenye vyumba 20, kila moja ina vitanda juu na chini (double-decker) ikihifadhi wanafunzi wanne, kila kitanda wawili.

Mkuu wa Shule, Emerenciana Luena, anasema wakati wa likizo wanafunzi wanakuwa huru makwao, ikizingatiwa wazazi na walezi wanakuwa shambani na shughuli zingine za kiuchumi.

Anasema kufunguliwa shule baada ya likizo ya corona wiki ya kwanza wamekutana na mahudhurio duni, sehemu kubwa ni wasichana.

Mkuu wa Shule anawasilisha picha halisi kwamba wiki hiyo pekee, alipata taarifa mabinti 40 walitoroka na walipofuatilia undani wake, waligundua wengi ni wa kidato cha kwanza hadi tatu, wametoweka kusikojulikana.

Luena anakariri ufafanuzi wa wazazi walipoulizwa, walidai walitoroka pindi walipokuwa kwenye shughuli na wengine walitoroka usiku na nguo zao.

"Kuna kesi hapa ilikuja mtoto katoroka na kukamatwa ndani ya basi akilekea Dar es Salaam, baada ya kukamatwa alirejeshwa nyumbani kwao.

"Alikaa nyumbani kwa muda wa siku tatu na siku iliyofuata akatoroka moja kwa moja hadi leo," anaeleza Luena, akitaja wengi hukimbilia miji mikubwa Dar es Salaam, Mwanza na Arusha.

Anataja mkasa wa pili, mwanafunzi wa kidato cha pili alitoroka kwao mwezi Mei iliyopita akiwa likizo na alirudi shuleni siku tatu kabla ya shule kufungua, akigundulika kuwa na mimba ya miezi miwili.

Aliwashauri wazazi wake kuripoti polisi na wenyewe wakifuatilia kinachoendelea.

Luena anaeleza kwa masikitiko mkasa wa mwanafunzi aliyemlea nyumbani kwake na kusoma mahali hapo na sasa yuko kidato cha sita, mama yake alimuacha kuhudumia baa wakati wa likizo, aliangukia maambukizi ya virusi vya ukimwi, baada ya kufanyiwa ukatili na baba wa kambo, pindi mama alipoenda kwenye biashara.

Pia anasimulia mwaka juzi msichana alipata mimba akiwa kidato cha nne, ila kwa bahati mbaya mtoto wake alifariki.

Anasema, alimshawishi kuendelea na masomo na kupitia mfumo usio rasmi na akakubali, kwani shule yake ni kituo cha mitihani cha Baraza la Mitihani la Taifa (Necta).

Mwalimu Luena, anataja sababu mojawapo za mabinti hao kuangukia kwenye ngono isiyo salama na hata mimba ni kutengana kwa wazazi, hata watoto wanajikuta na uhuru uliopitiliza maishani, akitoa mfano wa kulelewa na bibi.

Anasema baada ya likizo ya mwezi Desemba iliyopita, wanafunzi wa watatu walipimwa na kukutwa na ujauzito, wiki ya kwanza baada ya shule kufunguliwa.

Pia, anataja watoto kubebeshwa majukumu ya kifamilia hasa za mama za wanaoshinda kwenye vilabu vya pombe na kurudi usiku, mabinti wakikosa usimamizi majumbani.

Kuhusu hatua wanazichukua, anasema hivi sasa wanataka kupata idadi kamili ya waliopata mimba muda wowote kwa upimaji wa kushtukiza shuleni hapo.

"Kwa wiki hii ya kwanza tunawaacha ili idadi iweze kuongezeka, kwa sababu wanajua mipango yetu kuwa kila baada ya likizo tunawapima mimba."

### HADAA KWA MABINTI

Mwalimu Luena anaendelea kuwa: "Kutokana na shule yetu kuwa karibu na barabara kuu ya magari na mabasi makubwa yaendayo mikoani, wasichana wengi hushawishiwa kwa kupewa lifti muda wa kwenda na kurudi shuleni." Anasema alioazimika kuitisha kikao cha wazazi kuwahadharisha wasichana wasionekane stendi ya mabasi kujiepusha na lifti za madereva.

Pia anawataja waendesha bodaboda wanaotumia kigezo cha kusaidia wanafunzi lifti asubuhi na jioni, ikiambatana na hadaa za zawadi kama nguo za ndani, fedha za chipsi na soda.

"Hali duni kimaisha, umbali wa shuleni, pia ni changamoto zingine kwa wasichana, kwani wengi wanawaza asubuhi akichelewa mwalimu atamchapa viboko na jioni akichelewa mzazi au mlezi atamchapa, hivyo wanaona suluhisho ni kuomba lifti kwa wenye bodaboda," anaeleza mwalimu.

Anafafanua, kuwa licha elimu ya uzazi na magonjwa ya zinaa kama ukimwi kutolewa kwa wanafunzi wote shuleni, bado ugumu wa maisha na umbali wa shule unawashawishi vinginevyo kwenye ngono.

### KILIO HOSTELI

Mkuu huyo wa shule anasema aliitisha kikao cha wazazi washirikiane na kamati ya shule kuwashawishi walipie watoto Sh. 83,000 za hosteli inayomilikiwa na kata na kujenga vyumba zaidi, lakini mwamko ulikuwa mdogo.

"Tuna wanafunzi zaidi ya 350 na uwezo ni wanafunzi 80 tu," anasema na kuongeza ni tiba mojawapo dhidi ya tatizo la mimba kwa wanafunzi, huku hitaji hilo likiwagusa pia wavulana, kwa sababu wengi nyumbani wanafanyishwa vibarua kubeba mizigo ili kupata kipato cha kupanga jirani na shule.

Mwalimu anataja hatua kwa wavulana ambao kuna wakati hukimbia masomo kwenda kufanya vibarua, aliamua kuwapa baadhi ya vyumba vya vya maabara shuleni walale na kusoma.

### SHULE NEW KIOMBOI

Katika Shule ya Sekondari New Kiomboi, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Mkuu wa Shule, Amadeus Kiduu, anasema kutoka likizo ya ugonjwa corona shule ilipofunguliwa tarehe 29 mwezi uliopita, mahudhurio yalikuwa duni, wengi wanadaiwa kuwa na udhuru nje ya mkoa.

Pia kuna mkasa msichana mwenye miaka 14 alitoroka nyumbani wiki moja kabla ya kufungua shule, taarifa zilzowasilishwa na baba yake.

Mkuu huyo wa Shule anaeleza alimshauri mzazi kwenda kwa Mwenyekiti wa Kitongoji kutoa taarifa na baadaye polisi.

Baba wa mtoto aliiambia Nipashe katika ofisi za shule hiyo, kwamba binti alitoroka jioni saa moja na hadi wakati huo, haijulikani hata kwa ndugu zake wote mahali alikoo.

Hata hivyo, Ofisa Elimu Sekondari Iramba, Mwanjala Godfrey, alipohojiwa na Nipashe anakana kwa madai taarifa zilizoko mwanafunzi huyo ni mjauzito na ametoroshwa.

Godtrey anasema mimba za wanafunzi zimekuwa tatizo sugu, akiwanyooshea kidole malezi duni, pia wazazi kuficha mikasa wanachangia yanayotokea.

Anasema imebainika kuwa, wazazi wanakubaliana na wanaowapa mimba mabinti, tabia inayochangia usugu huo wa majanga, akitoa mfano baada ya likizo ya Desemba, waliwapima wanafunzi wa shule mbalimbali na walipatikana wajawazito 19 wa vidato vya pili na tatu.

Pia mwaka jana walimu watatu walifikishwa mahakamani kwa mikasa ya kujihusisha na mapenzi na mwanafunzi na wapo waliohukumiwa vifungo hadi miaka 30.

Anasema, ofisi yake kwa kushirikiana na wakuu wa shule za sekondari, wataendesha upimaji mimba kwa kushtukiza shuleni, huku Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa Iramba, Linno Mwageni, akisema wananunia kuufanya wa kudumu.

Mwageni anayekiri madhara ya likizo ya corona, anasema upimaji utafanyika kwa siri wakishirikiana na polisi kila baada ya shule kufunguliwa.

# JUA LINAVYOSHANGAZA

## ■Hatimaye picha karibu na jua zapatikana
## ■Zapigwa kilomita milioni 77 kutoka liliko

**Na Mwandishi Wetu**

NI jaribio lenye kufurahisha watu wengi baada ya dunia kuifanya kuwa karibu zaidi na jua tangu kupita karne nyingi.

Tangu wanasayansi kuanza kuchunguza mfumo wa anga za juu, hawakufanikiwa kupata picha zilizopigwa karibu na jua, hivyo kusababisha kazi yao kuwa ngumu.

Hata hivyo, picha za hivi karibuni ambazo zilizopigwa kutoka umbali wa kilomita milioni 77, umbali ambao ni karibu sana kuwahi kupigwa na kamera, zimeleta furaha kwa wanasayansi hao ambao wanaofuatilia mwenendo wa sayari zilizo katika mfumo wa jua.

Picha hizo kutoka Shirika la Anga la Ulaya ambazo zilichukuliwa kupitia setilaiti ya kuchunguza jua iliyorushwa mapema mwaka huu, imeibua mtazamo mpya kuhusu umri na mfumo wake wa kujiendesha.

Katika uchukuaji wa picha hizo, miongoni mwa vitu vilivyonaswa ni mwonekano wake mdogo.

Kwa kawaida mamilioni ya miako ya jua ambayo kawaida huonekana kwa kutumia darubini kutoka ardhini.

Lakini muwako huu mdogo mno huenda unahusika na mchakato wa joto unaofanya eneo la nje la jua au tabaka la mzingo kuwa na joto zaidi.

"Jua lina eneo lenye baridi la takriban selsiasi 5,500 na limezingirwa na eneo lenye joto kali zaidi ya selsiasi milioni," anaeleza mwanasayansi Daniel Müller.

Setilaiti ya Shirika la Anga la Ulaya, ilirushwa kupitia roketi kutoka eneo la Cape Canaveral, Marekani Februari mwaka huu.

Lengo lake lilikuwa ni kubaini siri iliyopo katika mzunguko wa jua.


Jua pamoja na kuwa na makujumu mengi, lakini muhimu ni kusaidia sayari kuwa kwenye mhimili wake pamoja na kutoa mwanga na joto.

Wakati wa mchakato wa uwakaji wake, mara nyingi huwa kuna chembechembe zinazoruka kutoka uga sumaku wa jua kupitia kwenye setilaiti na kuharibu mawasiliano ya redio.

Lakini kwa uvumbuzi huu unaweza kusaidia wanasayansi kutabiri vizuri mwingiliano huo.

"Hali ya hivi sasa ya ugonjwa wa virusi vya corona imeonyesha umuhimu wa kuwa na mawasiliano na setilaiti ni sehemu ya mawasiliano," amesema Caroline Harper, Mkuu wa Shirika la Anga la Uingereza.

"Kwa hiyo ni muhimu sana kuendelea kufahamu mengi kuhusu jua ili tuweze kubashiri hali ya anga iliyopo kwenye jua kama tulivyojifunza kubashiri hali ya hewa hapa duniani." Anaongeza.



Chombo cha kuchunguza jua kimewekewa mfululizo wa mizunguko karibu na jua, na hatimaye kitafika umbali usiozidi kilomita milioni 43.

Picha zilizoonyeshwa siku ya Alhamisi ya wiki iliyopita, zimepigwa katika eneo hilo karibu na jua linalofahamika kama perihelion kwa kitaalamu.

Matukio yote yalitokea katikati ya Juni mwaka huu ndani ya mzunguko wa sayari ya Venus.

Kwa ulinganisho, Dunia ipo takribani kilomita milioni 149 sawa na (maili milioni 93) kwa wastani kutoka kwenye jua.

Wataalamu hao wanasema picha hizo za karibu zaidi na jua kuwahi kupigwa, zimepatikana sio ndio wamepata mafanikio makubwa.

Itachukua miaka kadhaa kabla ya chombo cha jua kupiga picha zingine za karibu zaidi umbali wa kilomita milioni 48 kutoka uso wa jua.

Wakati mchakato huo unaendelea, kupitia Shirika la Anga la Ulaya pamoja na nguvu za uvutano za nyota ya Venus, chombo kinachochunguza jua kitakuwa kinajiondoa kwenye nyota ili kiweze kuona kwa urahisi zaidi, tabaka la jua lenye mashimo ambalo lina hali ya baridi lenye kubadilika badilika.

Katika eneo hilo, huenda hatimaye dunia ikafahamu mambo ya msingi kuhusu nguvu za sumaku za jua.


"Tunajua kwamba uga sumaku wa jua ndio unaosababisha yote yanayotokea kwenye jua, lakini hatujui jinsi uga sumaku unavyotengenezwa," anaeleza mwanasayansi huyo kutoka Taasisi ya Utafiti wa mfumo wa jua.

"Tunafikiria kwamba huenda ikawa ni mfano wa mota inayofanya hivyo ndani ya jua, kama ilivyo ndani ya dunia. Lakini hatujui jinsi inavyofanyakazi," anasisitizaGilbert.

Ana matumaini makubwa na hatua zitakazopigwa siku za usoni katika sayansi.

"Ikiwa tayari tumeshabaini kitu kwenye picha za kwanza za mwanga tulizopiga, fikiria ni kitu gani tutakachogundua tutakapokaribia zaidi jua, na tutakapotoka nje ya ekliptiki. Ni jambo linalosisimua sana." Anasema mwanasayansi hiyo.

KWA MSAADA WA MITANDAO



# Afrika Kusini yafunga tena shule kudhibiti corona

**PRETORIA, Afrika Kusini**

AFRIKA Kusini imezifunga shule kwa wiki nne kuanzia Jumatatu ya wiki inayokuja kama njia ya kukabiliana na ongezeko la maambukizi ya virusi vya corona.

Hatua hiyo ambayo imechukuliwa kwa mara ya pili tangu kuanza kusambaa kwa virusi vya corona, Rais wa nchi hiyo, Cyril Ramaphosa, katika hotuba yake aliyotoa juzi, alisema ilikuwa muhimu kufunga shule ili kuhakikisha zisigeuke kuwa vituo vya maambukizi.

Uamuzi wa kufunga shule unatokana na Baraza la Utafiti wa Matibabu Afrika Kusini, kutoa takwimu zikionyesha watu waliokufa na corona imefikia 17,000, sawa na asilimia 59 zaidi ikilinganishwa vifo vilivyotokea miaka ya nyuma.

Idadi ya watu wanaokufa kwa muda wa saa 24, imefikia 572 idadi ambayo imetajwa kuwa ya juu.

Shule za msingi na sekondari zilifunguliwa tena Julai 6.

"Kwa kuzingatia maoni ya wadau na wataalamu mbalimbali, baraza la mawaziri limeamua kwamba shule zote za umma zitachukua mapumziko ya wiki nne," alisema Ramaphosa.

Alisema kuwa mwaka wa masomo utaongezwa hadi mwakani kwa sababu ya janga la corona.

"Tumechukua njia ya tahadhari kufunga shule kipindi hiki ambapo nchi inatarajiwa kupata maambukizi ya juu zaidi," alisema.

Aidha, Rais pia ametangaza mfuko wa fedha wa dola bilioni 30 sawa na pauni bilioni 24 kufadhili huduma za afya na kusaidia wenye uhitaji.

Hata hivyo, idadi ya watu waliokufa huenda ikawa ya juu zaidi ya ile inayotangazwa.

Afrika Kusini imeshika nafasi ya tano duniani kuwa na idadi kubwa ya watu waliopata maambukizi kwa kuwa na wagonjwa 400,000 na vifo 5,940.

**BBC**



Mgonjwa wa Covid-19 akisubiri kupata matibabu nje ya Hospitali ya Jimbo la Honorio Delgado, nchini Peru, baada ya huduma ya matibabu kuelemewa. **(PICHA: AFP)**

# Trump afuta mkutano kuhofia corona

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amefuta kongamano la chama chake cha Republican, katika Jimbo la North Carolina, baada ya kuongezeka kwa maambukizi ya Covid-19.

Trump alikuwa amehamisha sehemu ya mkutano huo Florida kwa sababu ya kanuni za kutokaribiana zilizoanzishwa North Carolina.

Mkutano huo unaotarajiwa kufanyika Agosti 24, sasa umehamishiwa Jimbo la Florida, utakuwa maalumu kwa ajili ya kumchagua Trump, kupeperusha bendera ya chama hicho kwa mara ya pili.

Hata hivyo, baadhi ya wajumbe wa chama cha Republican wataendelea kukutana Charlotte, North Carolina, eneo ambalo mkutano huo ulikuwa umepangwa kufanyika awali.

Kiongozi hiyo ameamua kuchukua hatua hiyo baada ya jimbo hilo kuweka kanuni mpya za kutokaribiana kwa ajili ya kukabiliana na wimbi jipya la kusambaa kwa virusi hivyo.

Katika mkutano wake uliofanyika Ikulu, Trump, alisema kuwa usalama ndio jambo muhimu kwake na alitoa wito wa kufutwa kwa matamasha manne ya usiku.

"Ni dunia tofauti, na hali hii itaendelea kwa muda kidogo, nilihisi kufanya hivyo itakuwa makosa na kuhatarisha maisha ya maelfu ya watu," alisema Trump.

Aliongeza "Hatutaki kuhatarisha maisha hata kidogo, ni lazima tuwe waangalifu. Lazima tuwe makini na tuwe mfano wa kuigwa na wengine."

Ofisi ya Jacksonville Sheriff shirika la kaunti linalosimamia utekelezaji wa sheria lilionya wiki hii kwamba mji huo hauko tayari kwa mkutano mkubwa wa kisiasa uliopangwa kufanyika mwezi ujao.

Hata hivyo, maofisa wa Chama cha Democratic, wamekejeli tangazo la rais huyo, wakisema limechelewa na inaonyesha jinsi gani kiongozi huyo hayupo makini na afya za watu.

**BBC**

# China yalipiza kisasi, yafunga ubalozi

**BEIJING, China**

CHINA imeiamuru Marekani kuufunga ubalozi wake mdogo katika mji wa magharibi wa Chengdu.

Hatua hiyo imechukuliwa kama kulipiza kisasi baada ya Marekani kuagiza kufungwa kwa ubalozi mdogo katika mjini Houston wiki hii.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya China, Wang Wenbin, alisema Marekani inatakiwa kulaumiwa kutokana na mgogoro huo.

Rais Donald Trump, aliamuru kufungwa kwa ubalozi huo mdogo wa China ndani ya saa 72, akidai maofisa wa China walijaribu kuiba data kutoka katika Taasisi ya Sayansi ya Matibabu ya Chuo Kikuu cha Texas A&M.

Marekani imeishutumu China kwa wizi huo wa taarifa za kitaaluma, siku moja baada ya wizara ya sheria kuwafungulia mashtaka raia wawili wa China kwa madai ya kudukuwa kampuni kadhaa za nchi hiyo na kujaribu kuiba utafiti wa chanjo ya virusi vya corona.

**DW**

# Viongozi Afrika washindwa kutatua mgogoro wa Mali

**BAMAKO, Mali**

VIONGOZI wa nchi za Afrika Magharibi wamemaliza mkutano wa kushughulikia mgogoro wa uongozi wa Mali, bila kufikia makubaliano.

Viongozi wa nchi tano za ukanda huo (ECOWAS) walikutana na kuzungumza na Rais wa Mali, Ibrahim Boubacar Keita, na viongozi wa vuguvugu la maandamano wanaomtaka ajiuzulu. Hata hivyo, upatanishi huo uliofanywa na Rais wa Niger Mahamadou Issoufou, pamoja na wenzake wa Senegal, Ivory Coast, Ghana na Nigeria walishindwa kupata suluhu.

Hata hivyo, mkutano mwingine umepangwa kufanyika Jumatatu.

Viongozi wa kundi la vuguvugu linaloitwa Juni 5, wanamtaka Keita, aondoke madarakani kwa kushindwa kuushughulikia uchumi ulioporomoka, ufisadi na uasi wa miaka minane wa makundi ya kijihadi.

**DW**

# HADITHI

# Mauaji Harusini-22


ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**




"Umeagiza chakula?" Shani aliuliza.

'Nilikuwa nakusubiri ili uagize. Mimi nitakula chakula ambacho wewe utakula."

Shani alitabasamu na uzuri wake ukaongezeka.

Ghafla, kati yao alisimama kijana yule yule ambaye aliangusha kifuko ambacho Eddy aliona kama ni sumu.

Alikuwa amefika pale muda sekunde chache tu baada ya Shani kufika.

"Niletee chakula changu ninachokipenda." Shani alimwambia kijana yule ambaye walionekana kuwa wamezoeana.

"Hapana." Eddy aliingilia kati.

"Nimeshaagiza chakula kwa mhudumu mwingine wewe unaweza kuendelea kwenye meza zingine." Aliongea kwa sauti ya upole.

Shani na mhudumu yule ambaye hakuwa mwingine ila ni Fikiri walipatwa na mshangao. Fikiri pamoja na mshangao, lakini pia alishtuka.

"Hapana nakutania rafiki yangu, lete hicho chakula." Eddy aligeuka, ikiwa na nia ya kuwaondoa kwenye mshangao na kuonyesha kuwa alikuwa akiwatania. Shani na Fikiri walifikiri hivyo.

Kwa upande wa Fikiri ilikuwa ni kama bahati hivi, kwani alianza kuwaza kama jambo lake lisipofanikiwa angefanya nini, kwani angelazimika kurudisha pesa kwa wenyewe.

Maneno ya mwisho ya Eddy walimrudisha kwenye furaha na haraka alitoka kwenda kuleta chakula alichoagizwa na Shani.

Eddy naye alinyanyuka na kuelekea kama anakwenda msalani, lakini alipofika katikati alikutana na mhudumu wa kike akamsimamisha. Waliongea kwa sekunde kadhaa, kabla ya kuelekea msalani haraka, akarejea.

Wakati huo, ndipo mhudumu Fikiri alikuwa anafikisha chakula kwenye meza aliyokuwa amekaa Shani.

Eddy alifika muda huo huo. Hakutaka kabisa Shani aguse kile chakula. Tayari kengele ya hatari ilishaanza kulia kwenye kichwa chake.

"Huyu ndiye aliyeangusha kifuko chenye sumu. Je, kwa nini hiyo sumu awe nayo mfukoni mwake, tena kipindi hiki cha kazi? Ni kwamba kilikuwa mfukoni kwa bahati mbaya? Na kama si kwa bahati mbaya, mhudumu huyu alitaka kuifanyia nini? Je, kuna mtu analengwa kuwekewa sumu kwenye chakula? Je, ni nani?"

Haya ndiyo maswali aliyokuwa akijiuliza Eddy kwa haraka haraka, ndiyo maana hakutaka kabisa Shani aguse chakula kile hata kama yeye si mlengwa.

Mawazo yake yalisitishwa na mhudumu mmoja wa kike aliyefika mezani akiwa na sinia yenye sahani mbili za chakula.

Ilikuwa ni aina ile ile ya chakula ambacho alikipenda Shani. Mshangao ukampata Shani kuona kuna sahani nyingine mbili, baada ya ile moja.

Eddy alisongeza sahani moja kwa Shani na nyingine akaisogeza kwake. Ile nyingine akaisogeza pembeni.

"Hiki tutakula baadaye kama hatukushiba." Alisema akimtazama Shani kwa tabasamu jepesi.

"We mambo yako bwana. Yaani sahani tatu zote za nini hizi?"

"We hunijui, mimi nakula sana, kwa hiyo naweza nisishibe sahani hii moja, nikaongeza na hii, wewe pia inaweza usishibe, tukagawana nusu kwa nusu."

"Mimi." Shani aliongea akijishika kifua "Wala, mimi si mlaji sana, hii hii tu inaweza kunishinda. Halafu si tungeagiza mbili, halafu kama hukushiba ukaagiza? Haya angalia sasa maana watu wakiona hivi wanatucheka, wanajua du hawa watu wanakula sana."

"Kwani wewe unaangalia watu? Mbona mimi nakuangalia wewe tu?"

Shani hakujibu kitu, alitabasamu na kuangalia chini. Kwa upande wake tukio hilo aliliona ni kama mwendelezo tu wa vituko vya Eddy.

Kwake alimuona na mwanaume mzuri, mchangamfu, mwenye akili, busara, vituko na mzaha mwingi.

"Enhe niambie mrembo wangu, malkia wangu ninayekupenda kama uaridi jekundu." Eddy alivunja ukimya.

"Mhh umeanza hivyo." Shani alijibu, akiwa kama vile hakupenda Eddy aongee maneno hayo, kumbe sivyo.

Hakuna binadamu yoyote duniani asiyependa kusifiwa, hususan viumbe wanaoitwa wanawake.

"Nashukushuru kusikia hivyo." Alijibu kivivuvivu na kwa madaha, huku akikata kipande cha nyama na kukitia kinywani.

"Siku ile tuliongea sana kwenye simu, sasa leo tuko laivu na wewe mwenyewe ndiyo ulinialika hapa, nataka kusikia yale maneno uliokuwa unaongea kwenye simu hapa."

Shani alimuangalia Eddy kwa jicho la huba, lililochanganyika na jicho linalomuambia kuwa yale aliyokuwa anaongea hayajabadilika.

"Siwezi kuongea tena kama yale yale kwenye simu siku ile Eddy, ila tu cha kukuambia ni kwamba wewe umekuwa sehemu kubwa ya furaha yangu kwa sasa.

""Kwa nini?"

"Kwa muda mrefu nimekuwa kama sina furaha hivi kwenye maisha yangu na hasa baada ya mama kufariki nikiwa bado mdogo, nimeishi kwenye familia ya kitajiri nikipata kila kitu, lakini faraja na amani ya moyo nilikuwa sina hadi nilipokutana na wewe siku ile."

"Shani ni kitu gani ambacho wewe unadhani mimi ninacho kilichokufanya sasa uwe na furaha na amani?" Eddy alizidi kumchimba mwenzake.

"Sijui, basi tu. Tangu siku ile makaburini tulipokutana, ulipoondoka na mimi kuondoka, niliona kabisa kama moyo wangu umekuwa unahitaji kukufahamu zaidi na hata ulipoanza kuwa unanisalimia na kuwasiliana na mimi, kusema kweli moyo wangu ulionyesha unakuhitaji sana."

Eddy alitazama Shani kwa makini na kugundua kuwa anachokisema kilitoka rohoni na si mdomoni.

"Leo nitapenda kukwambia kitu kimoja tu. Shani nakupenda sana zaidi ya neno lenyewe na naahidi nitaendelea kukupenda na kukujali siku zote. Na hii siyo kwa sababu wewe unasema umekuwa na faraja na amani ya moyo kuwa na mimi, ila nilipokuona kwa mara ya kwanza tu kule makaburini moyo wangu ulikuwa tayari umeshawaka juu yako, naahidi nitakupenda na sitokuangusha au kukukwaza."

Taratibu machozi yalianza kumtoka Shani. Alijisogeza karibu na Eddy akamkumbatia. Akajilaza kifuani.

"Usinione hivi Eddy, mimi nimekuwa na matatizo makubwa. Na hadi leo bado nina matatizo makubwa. Na sikuwa na mtu yoyote wa kushea naye matatizo yangu. Wewe ni rafiki yangu, naomba tuwe pamoja kwenye furaha na matatizo yangu," alilia Shani.

"Najua. Najua Shani. Tutakuwa wote. Sitokuacha peke yako. Ila kuna siku ningependa uniambie matatizo yote yaliyokupata huko nyuma, yaliyokuwapo na ambayo unaona kama yatakuwa kikwazo kwako."

"Nitakwambia, lakini siyo hapa. Nitakwambia sehemu maalum. Tukiwa wawili tu.

***Itaendelea Jumamosi***

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;198/2020**

Ombi la THERESIA NICHOLAS SHAYO,-Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NICHOLAS BENEDICT SHAYO.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/07/2020.

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 118/2020**

Ombi la VALENCE JOSEPH KISHE kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu ADELINA CRISTOSIA SHIRIMA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 10/08/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 24/07/2020.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

RICHARD NALBAT MAHENGE anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili MC.830 AUW aina ya TVS KING.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi MBE/MBE/RB/554718/2020

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI.

**CRAIG PACKER** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 675 AHA Toyota Prado.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi:

Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/525426/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEOFREY HENRY SELEMAN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato ch nne chenye index namba S1127/0094 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Bugando.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**NZ/RB/48000/2019**


Uza, Chenye Thamani Kubwa

Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## THIAGO: SIKUTAKA KUONDOKA PSG

**PARIS, Ufaransa**

THIAGO Silva hataki kuondoka Paris Saint-Germain, lakini amesema huu si wakati sahihi kwa yeye kujadili jambo hilo la kuondoka.

Mlinzi huyo wa kati wa Brazil, Silva alikubali kubaki na mabingwa hao wa Ligue 1 kwa ajili ya fainali za Coupe de France na Coupe de la Ligue, pamoja na kuisaidia PSG kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Agosti, licha ya kuthibitisha mwezi uliopita kwamba ataondoka mwishoni mwa msimu huu.

Mkongwe Silva amejiimarisha yeye mwenyewe kama gwiji wa klabu hiyo tangu alipotua hapo akitokea Milan mwaka 2012 na amecheza mechi 300 kwa miamba hao wa Ligue 1.

Silva aliagwa kwenye mchezo wa kirafiki wa ushindi wa 4-0 dhidi ya Celtic pale Parc des Princes wiki hii, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 35, alikuwa akitaka kubaki kwenye timu hiyo kwa malengo ya kushinda nayo mataji.

"Ni wakati wa aina yake kwangu. Pamoja na mashabiki, mara zote tumekuwa tukiheshimiana. Waliniuliza kama nitaweza kubaki, lakini si maamuzi yangu. Sasa si wakati wa kuzungumzia jambo hili," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tutakuwa na muda wa kuzungumza kuhusu hilo baadaye. Sikutaka kuondoka, lakini maamuzi tayari yameshafanywa. Naheshimu maamuzi na nitayaheshimu hadi mwisho."

## JUVENTUS IMECHOKA KIAKILI NA NGUVU - SARRI

**TURIN, Italia**

MAURIZIO Sarri anaamini Juventus "wamechoka kinguvu na akili" baada ya kukutakana na kipigo cha kushangaza kutoka kwa Udinese, Alhamisi.

Baada ya Matthijs de Ligt kuiweka mbele Juve na kuwa kwenye nafasi nzuri ya kuelekea kulitwaa taji la Serie A, Udinese iliyopo kwenye hatari ya kushuka daraja iliwashangaza.

Ilija Nestorovski alisawazisha bao kabla ya Seko Fofana kufunga la ushindi dakika ya 92, na kuwaacha Juve wakiwa kileleni kwa pointi sita, huku zikiwa zimebakia mechi tatu ligi kumalizika.


Sarri alikilaumu kikosi chake huku akisema ratiba imekuwa ngumu kwao kwa kucheza mechi sita mwezi huu.

"Kwa kipindi hiki, tumechoka kiakili na kinguvu, na hili ni tatizo la kawaida," alisema kocha huyo wa Juventus.

"Kwa sababu hii, tunatakiwa kujiimarisha na kujifua kwa ajili ya mechi zilizobaki kwa sababu hazitakuwa rahisi kwa upande wetu.

"Ni ngumu kucheza kwa kasi ile ile katika kila mechi na wakati mwingine mambo yanakuwa magumu kama mchezo huu, kwani tumepoteza."

Juve watakuwa na nafasi ya kutwaa taji la ligi hiyo kwa mara tisa mfululizo wakati watakapocheza dhidi ya Sampdoria, Jumapili.





# SANE
## ADOKEZA USAJILI WA HAVERTZ CHELSEA

**MUNICH, Ujerumani**

NYOTA mpya wa Bayern Munich, Leroy Sane amedokeza kwamba, uhamisho wa Kai Havertz kutoka Bayer Leverkusen kwenda Chelsea umekamilika.

Havertz mwenye umri wa miaka 21, anatarajia kuondoka kwa klabu hiyo ya Bundesliga kipindi hiki cha majira ya joto baada ya kuwa na msimu wa kuvutia.

Chelsea imeripotiwa kwamba ndiyo timu inayoongoza kwenye mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, huku tayari kikosi hicho cha kocha, Frank Lampard kikiwa kimeshamnasa Timo Werner na Hakim Ziyech kwa ajili ya msimu ujao.

Sane, ambaye aliwasili hapo Bayern akitokea kule Manchester City, amebainisha kwamba dili hilo tayari limeshafanikiwa, wakati akiwazungumzia wachezaji hao wawili vijana wa Ujerumani.

"Nafikiri mara zote Ujerumani ina wachezaji wazuri zaidi vijana, hakuna swali kuhusu hilo. Sijui kwa nini (klabu) zinawaangalia sana wachezaji wetu vijana," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafikiri Bundesliga mara zote inavutia, unaweza kuona wachezaji vijana wanapata nafasi na kuimarika vizuri kwenye Bundesliga. Haijalishi ni klabu gani.

"Bila shaka, kwa usajili wa Timo Werner na Kai Havertz - wachezaji wawili wenye mwaka mmoja kwenye ligi - Chelsea imefanya kazi nzuri. Hakuna swali kwamba Ujerumani ina program nzuri sana ya wachezaji vijana.

"Nafikiri dunia nzima inajua wapi kwa kuwapata wachezaji vijana wazuri zaidi, ni Bundesliga pekee ndiko unaweza kuwapata wachezaji hao."




# KIWANGO

## CHA NEYMAR CHAMKUNA TUCHEL PSG

**PARIS, Ufaransa**

KIWANGO cha Neymar tangu Paris Saint-Germain iliporudi dimbani hakijamshangaza kocha, Thomas Tuchel.

Tangu kurudi kutoka Brazil baada ya mlipuko wa vizuri vya corona, Neymar kwa haraka amekuwa kwenye kiwango bora wakati msimu ulipofutwa nchini Ufaransa.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, amefunga mabao manne kweye mechi tatu za kirafiki za ushindi dhidi ya Le Havre, Waasland-Beveren na Celtic, ambazo zilimalizika kwa ushindi wa 9-0, 7-0 na 4-0.

PSG walipewa taji la Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, baada ya msimu kufutwa Aprili na wanatarajia kushinda Kombe la Coupe de France fainali iliyochezwa jana Ijumaa dhidi ya Saint-Etienne.

Alipoulizwa kuhusu kiwango cha Neymar, Tuchel alisema: "Sishangai. Amerudi akiwa na mtazamo chanya na kiwango cha kuvutia.

"Amejiimarisha haraka kwenye mazoezi, na ameongezeka na ana kasi. Hilo ni jambo muhimu sana kwa upande wake. Alipewa nafasi nyingi ya kucheza."

PSG baada ya fainali hiyo ya Coupe de France, itacheza fainali nyingine ya Coupe de la Ligue Julai 31 dhidi ya Lyon, kabla ya kwenda jijini Lisbon kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo wamepangwa kucheza na Atalanta kwenye robo fainali.

## ARSENAL KUMKOSA MUSTAFI FAINALI FA

**LONDON, England**

SHKODRAN Mustafi ni majeruhi na kuna hofu kama atacheza fainali ya Kombe la FA, Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, amethibitisha.

Arsenal ilifuzu kucheza fainali hiyo baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Manchester City pale kwenye dimba la Wembley wiki iliyopita, ingawa walimpoteza mlinzi Mustafi aliyeumia nyama za paja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani aliukosa mchezo wa Alhamisi wa kipigo kutoka kwa Aston Villa na hatakuwapo kwenye mchezo wa mwisho wa Arsenal wa Ligi Kuu msimu huu dhidi ya Watford, Jumapili.

Na Arteta amejipanga kuwa bila mlinzi huyo wa kati mwenye umri wa miaka 28, katika mchezo wa fainali hiyo dhidi ya Chelsea, Agosti Mosi mwaka huu.

"Musti ameumia, bado hatujajua atakuwa nje kwa muda gani, lakini katika mechi zetu zijazo hatakuwapo," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Nina shaka kama atakuwa fiti kwenye fainali, tutaangalia kwa siku zinazokuja. Lakini kwa wakati huu sina uhakika kama atakuwapo."

Awali siku za Mustafi pale Arsenal zilionekana kuelekea ukingoni mwanzoni mwa msimu huu, lakini mchezaji huyo wa zamani wa Valencia ameimarika chini ya Arteta.

## EMERY KOCHA MPYA VILLARREAL

**VALENCIA, Hispania**

UNAI Emery ameteuliwa kuwa kocha mkuu mpya wa klabu ya Villarreal ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Kocha huyo wa zamani wa Arsenal, Paris Saint-Germain na Sevilla amesaini mkataba wa miaka mitatu na klabu hiyo, ambayo ilimaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa LaLiga msimu huu wa 2019-20.

Hii ni kazi ya kwanza ya Emery tangu alipofukuzwa kule Arsenal, Novemba mwaka jana baada ya kushinda mchezo mmoja tu kati ya tisa kwenye mashindano yote.

Alimrithi Arsene Wenger pale kwenye dimba la Emirates mwaka 2018, lakini alishindwa kuiwezesha Arsenal kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku pia akipoteza kwenye fainali ya Kombe la Ligi ya Europa kwa kufungwa 4-1 na Chelsea mwaka jana.

Emery amechukua nafasi ya Javier Calleja, ambaye ameondoka hapo Villarreal mwishoni mwa msimu huu, licha ya kuiwezesha kufuzu Ligi ya Europa.

"Sina malalamiko, lakini nimeumizwa," alisema akiiambia El Transistor. "Sasa ni wakati wa kurudi kwa Unai Emery na natumaini kuwapeleka juu kadri iwezekanavyo.

"Nimeumizwa kwa namna hii ilivyotokea. Ningeweza kufanya tofauti."

Villarreal ilipoteza mechi tatu kati ya tano za mwisho, lakini awali ilicheza mechi sita mfululizo bila kufungwa, na kuweza kuwarudisha kwenye Ligi ya Europa.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GIROUD KUMPIKU PLATINI UFARANSA

●●●Nilikuwa na nafasi ya kufanya hivyo kwenye fainali za Euro na wakati nikishinda...

**LONDON, England**

OLIVIER Giroud anapanga kumpiku Michel Platini kama mfungaji bora wa pili wa Ufaransa wakati mshambuliaji huyo wa Chelsea akiwa na nia ya kufikisha mechi 100 kwa Les Bleus hao.

Giroud ambaye alifika fainali ya michuano ya Euro 2016 na Ufaransa kabla ya kushinda Kombe la Dunia mwaka 2018, ameifungia timu hiyo ya taifa mabao 39 katika mechi 97.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33, amekuwa sehemu ya kikosi cha kocha Didier Deschamps na anahitaji mabao matatu tu kuweza kumpiku Platini na kushika nafasi ya pili kama mfungaji bora wa wakati wote wa Ufaransa, nyuma ya Thierry Henry, aliyefunga mabao 51 kati ya mwaka 1997 na 2010.

Sasa, Giroud ameweka nia yake ya kuchukua nafasi ya Platini kwenye historia ya ufungaji wa kikosi cha Ufaransa.

"Nilikuwa na nafasi ya kufanya hivyo kwenye fainali za Euro na wakati nikishinda Kombe la Dunia," alisema kwenye mahojiano na Canal+. "Bado nina kiu ya mataji na kuvunja rekodi kwenye timu ya Taifa ya Ufaransa.

"Itakuwa vizuri kufikisha mechi 100, na kumpiku Platini kwenye nafasi ya pili kwa ufungaji mabao.

"Kuna mabao na michuano ya Euro mwakani, bila shaka nitaweza kufanikisha hilo kwa haraka."

Giroud alifunga mabao sita kwa Ufaransa wakati ikiwania kufuzu kwa Euro 2020, lakini michuano hiyo iliahirishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona na sasa itafanyika mwakani.

## KWA UFUPI

**BERGKAMP KUGEUKIA UKOCHA**

GWIJI wa Uholanzi na Arsenal, Dennis Bergkamp amesema ataangalia uwezekano wa kurudi kwenye soka kama kocha kwa siku za usoni. ***(FourFourTwo)***

**TORRES ABANIWA CITY**

VALENCIA imekataa kushusha bei ya ada ya uhamisho ya winga wake, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 21, wakati Manchester City ikiwania kumsajili nyota huyo wa timu ya Taifa ya Hispania chini ya umri wa miaka 21. (Telegraph)

**CHELSEA KWA GIMENEZ**

CHELSEA imekuwa ikimkodolea macho mlinzi wa Atletico Madrid na timu ya Taifa ya Uruguay, Jose Gimenez mwenye umri wa miaka 25, huku kocha Frank Lampard akionyesha nia ya kutaka kuimarisha safu yake ya ulinzi. ***(Telegraph)***

**SANE: HAVERTZ WA CHELSEA**

LEROY Sane mwenye umri wa miaka 24, ameonyesha kuthibitisha kwamba, nyota mwenzake wa timu ya Taifa ya Ujerumani, Kai Havertz mwenye miaka 21, anaelekea Chelsea kutoka Bayer Leverkusen kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Mail)***

**BRIGHTON KUIBANIA LEEDS**

KLABU ya Brighton haina mpango wa kumuuza mlinzi wake, Ben White mwenye umri wa miaka 22 kwa Leeds United, ambako amekuwa akicheza kwa mkopo msimu huu. ***(Mail)***

**ALCANTARA BEI JUU**

BAYERN Munich imesema kiungo wake wa kimataifa wa Hispania, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 29, hataruhusiwa kuondoka klabuni hapo kwa bei ndogo baada ya kuhusishwa kutakiwa na Liverpool. ***(Metro)***

**BENFICA KUMCHUNIA CAVANI**

KLABU ya Benfica imesitisha mpango wa kumshawishi mshambuliaji wa kimataifa wa Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 33, huku straika huyo wa zamani wa Paris St-Germain akiwa anataka pauni milioni 18 kwa msimu. ***(A Bola)***

**BALOTELLI AWANIWA COMO**

KLABU ya Serie C, Como imethibitisha kwamba ipo kwenye mazungunzo ya kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Manchester City na Liverpool, Mario Balotelli. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 raia wa Italia, anatarajia kuondoka katika klabu yake ya sasa ya Brescia. ***(La Provincia di Como, via Football Italia)***

**LINGARD AMUITA SANCHO**

JESSE Lingard mwenye umri wa miaka 27, amemshauri nyota mwenzake wa timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, kuondoka Borussia Dortmund na kujiunga naye kwenye kikosi cha Manchester United kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Evening Standard)***

**SPURS YATUA ROMA**

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia kiungo wa AS Roma na timu ya Taifa ya Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 21, ambaye wanawania kumsajili. ***(Guardian)***

**WEST HAM YAMTAKA EZE**

WEST Ham imemweka katika kipaumbele chake, kumsajili kiungo wa Queens Park Rangers, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 22, kipindi hiki cha majira ya joto, huku pia Crystal Palace ikimwania nyota huyo mwenye thamani ya pauni milioni 20. ***(Evening Standard)***



HABARI MICHEZO

# SABA ZAOMBEANA NJAA KUBAKI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20, ukitarajiwa kukamilika kesho Jumapili, macho na masikio ya mashabiki wa soka nchini ni kutaka kujua ni timu zipi zitaungana na Singida United kushuka daraja na gani zitakwenda kucheza mechi za mchujo ili kujua kama zitabaki au kuteremka moja kwa moja.

Jumla ya timu saba zipo kwenye vita kali ya kuhakikisha zinabaki Ligi Kuu, zikilazimika kushinda mechi za mwisho, huku zikiombeana mabaya, kila kitu ikiombea mwenzake afungwe ili awe salama.

Timu zilizopo kwenye hatari zaidi ya kushuka au kucheza mechi za mchujo ni Lipuli FC, Mwadui FC, Mtibwa Sugar, Mbao FC, Mbeya City, Alliance FC, na Ndanda FC.

Kati ya timu hizo saba, ndipo zitapatikana zikakazoshuka na zitakazokwenda kucheza mechi za mchujo na timu za Daraja la Kwanza, Ihefu FC na Geita Gold.

Mechi zitakazoangaliwa zaidi ni kati ya Mbao FC dhidi ya Ndanda itakayochezwa Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza.

Timu yoyote itakayofungwa kwenye mechi hiyo moja kwa moja itakuwa imeshuka daraja, kwani Ndanda yenye pointi 41 na inayokamata nafasi ya 19 itabaki hapo hapo, huku Mbao FC inayokamata nafasi ya 16, itasalia na pointi zake 42 ambazo zinaweza kabisa kupitwa na wenzake.

Sare yoyote kwenye mechi hiyo, inaweza kusababisha timu zote mbili kushuka daraja.

Mechi nyingine ni kati ya Alliance dhidi ya Namungo FC, ambapo wenyeji wakiwa Uwanja wa Nyamagana wanahitaji ushindi wa lazima ili kufikisha pointi 45 ambazo angalau zinaweza kuifanya kwenda kucheza mechi za mchujo badala ya kushuka moja kwa moja. Alliance inakamata nafasi ya 18, ikiwa na pointi 42.

Mtibwa Sugar ikiwa nyumbani, inatakiwa kuifunga Ruvu Shooting ili kufikisha pointi 45 zinazoweza kuifanya kuepuka kushuka daraja, au kuepuka hata kucheza mechi za mchujo, kwani ina pointi 42, lakini kati ya zote hizi yenyewe ina uwiano mzuri wa magoli ya kufunga na kufungwa.

Mbeya City, itakuwa Dar es Salaam kujaribu kupata pointi tatu kutoka kwa KMC, ili nayo ifikishe pointi 45 pia.

Lipuli inahitaji ushindi tu dhidi ya Yanga, ili iepuke moja kwa moja kushuka daraja na kucheza mchujo, kwani itafikisha pointi 47 ambazo timu nyingi za chini haziwezi kufikia, huku Mwadui ambayo nayo ina pointi 44, nayo ikihitaji ushindi dhidi ya Kagera Sugar.

ASILIMIA 10...




Mshindi wa Jackpot ya SportPesa, Jamal Abdallah, ambaye ameahidi kutoa asilimia 10 sawa na Sh. milioni 28.8 kusaidia watoto yatima nchini. **PICHA: SPORTPESA**

# Sven akunwa kiwango Simba Sc vs Coastal

**Na Somoe Ng'itu, TANGA**

BAADA ya timu yake kupata sare ya bila kufungana dhidi ya wenyeji Coastal Union, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck amesema amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake na kuongeza ni maandalizi mazuri kuelekea mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Namungo FC itakayochezwa wiki ijayo.

Kabla ya mchezo huo wa fainali, mabingwa Simba watashuka dimbani kesho Jumapili kufunga pazi la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika mjini Moshi.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Sven alisema mechi ilikuwa na ushindani wakati wote na ilidhihirisha kila upande unahitaji ushindi ili kulinda heshima baada ya kutobadilisha malengo.

Sven alisema imewasaidia kujiimarisha kuelekea mchezo wa fainali ya Kombe la FA na anatarajia kuona wanaendelea kucheza katika kiwango cha juu kesho na hatimaye kumaliza msimu kwa furaha.

"Ilikuwa mechi yenye ushindani kutoka kila upande, ingawa tulistahili ushindi, natumaini tutakuwa katika kiwango bora zaidi Jumapili na baadaye kwenye fainali ya FA, " alisema kwa kifupi Mbelgiji huyo.

Naye beki wa timu hiyo, Erasto Nyoni aliiambia gazeti hili mechi dhidi ya Coastal Union ilikuwa ngumu, lakini wanamshukuru Mungu waliimaliza salama na sasa akili yao inahamia kuifikiria Polisi Tanzania.

"Ingawa tulijiandaa kwa ushindi, lakini haikuwa hivyo, tulipambana sana na mwisho wa mchezo, tumegawana pointi, ndio soka lilivyo, hili tumelimaliza na akili yetu inaanza kufikiria mechi inayofuata, tunajua pia haitakuwa nyepesi, timu zote zimejipanga vizuri," Nyoni alisema.

Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili kuwa vijana wake wamefuata maelekezo yake ipasavyo na amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa katika mchezo huo wa raundi ya 37.

"Mechi ilikuwa nzuri sana, kwangu nawapongeza wachezaji wangu, wamepambana na wamefuata maagizo yangu kwa zaidi ya asilimia 80, naamini tutaendelea katika kiwango hicho kwenye mchezo wa mwisho hapo Jumapili," alisema Mgunda.

Mgunda alisema katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu hakukuwa na mechi rahisi kwa sababu ushindani ulianzia tangu mchezo wa kwanza na sasa umeongezeka kutokana na klabu kuhitaji kubakia kwenye ligi hii.

## Msiba wa Mkapa waahirisha Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limeahirisha mechi zote za Ligi Kuu Zanzibar kuanzia ratiba ya jana hadi hapo litakapotangaza vinginevyo kutokana na msiba mzito uliolikumba taifa, wa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benjamin William Mkapa, ambaye amefariki dunia usiku wa kuamkia jana hospitalini jijini Dar es Salaam alipokuwa kipatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa ratiba ya ligi hiyo, jana ilitakiwa kupigwa michezo mitatu ambayo ni Kipanga dhidi ya Selem View katika Uwanja wa Mau A, Polisi dhidi ya Chipukizi kwenye Uwanja wa Mau B, majira ya saa 10 alasiri huku majira ya saa nane mchana kulitakiwa kupigwa mchezo kati ya Mafunzo na Jang'ombe Boys katika dimba la Mau A. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Ali Ame Vuai, ilieleza kuwa klabu za Ligi Kuu zinatakiwa kusubiri mwongozo utakaotolewa juu ya mwendelezo wa mechi hizo za ligi katika kipindi hiki cha siku saba za maombolezo.

Ligi Kuu ya Zanzibar imebakisha michezo michache ili kukamilisha msimu huu ambapo hadi sasa hakuna timu inayoweza kujitabiria ubingwa.

## Mshindi SportPesa kusaidia yatima

**Na Hwandishi Wetu**

MSHINDI wa Jackpot ya SportPesa, Jamal Abdallah, mkazi wa Ilala jijini, Dar es Salaam aliyejishindia kiasi cha shilingi 288,974,720 ameahidi kutoa asilimia 10 ya fedha hizo sawa na shilingi 28,897,472 kusaidia watoto yatima nchini.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi jijini Dar es Salaam wiki hii, Jamal alisema fedha hizo ni nyingi sana na hakutegemea kushinda na alichokuwa akikitarajia zaidi ni kuibuka na bonasi kama ambavyo aliwahi kushinda bonasi ya Sh. milioni 12 mwaka jana.

"Namuamini sana Mwenyezi Mungu na ninaimani hii yote ni mipango yake, hivyo basi nimeamua kutoa asilimia 10 ya fedha hizi kama sadaka ambapo nitawagawia watoto yatima ili niweze kuwagusa kwa namna moja ama nyingine.

"Najua wengi watashangazwa na hili, lakini huu ni utaratibu nilioamua kujiwekea ili kuhakikisha nawafikia wenye uhitaji," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa Kampuni ya SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema: "Kusema ukweli hii ni mara ya kwanza kwenye historia kupata mshindi ambaye ameweka hadharani azima yake ya kutoa sadaka kwa kusaidia watoto yatima.

"Tunampongeza sana kwa maamuzi yake na tunamtakia kila la kheri, pia tungependa siku anayopanga kwenda kutembelea vituo hivyo atushirikishe na sisi ili kuweza kusaidiana kwa namna moja ama nyingine.

"Mtu yeyote anaweza kuibuka mshindi kwani mpira wa miguu matokeo yake hayajifichi, hivyo basi kwa ushiriki wake unathibitisha uaminifu wa hali ya juu kwa kampuni yetu."

# Michezo

Jumamosi Julai 25, 2020

Nipashe




Giroud kumpiku Platini Ufaransa HABARI UK 22



# TUTAKUKUMBUKA

## Samatta, wadau wa michezo waungana kumlilia Mkapa, aacha alama kubwa...

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa soka nchini na Watanzania kwa ujumla wameungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli pamoja na familia ya aliyekuwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa, ambaye amefariki dunia usiku wa kuamkia jana, kumlilia.

Mkapa ambaye alifariki dunia hospitalini jijini Dar es Salaam ambako alikuwa akipatiwa matibabu, pamoja na mambo mengi makubwa aliyoyafanya katika historia ya nchi hii, anakumbukwa zaidi na wadau wa michezo nchini kutokana na alama kubwa ya Uwanja wa Taifa aliyoiacha.

Ikumbukwe Uwanja wa Taifa ambao ulikamilika rasmi mwaka 2007 ukichukua watazamaji 60,000, ulijengwa kwa ushirikiano wa Serikali ya China na Tanzania chini ya Rais Mkapa wakati huo, kwa gharama ya Sh. bilioni 56. Hizo zikiwa ni juhudi za zake katika kuhakikisha sekta ya michezo nchini inakua kwa kasi.

Na juzi usiku wakati Rais Magufuli akitangaza msiba huo, aliwataka Watanzania wote kuwa watulivu na wastahimilivu baada ya kupokea taarifa za kuondokewa na mpendwa wao, Mkapa.

"Kwa masikitiko makubwa tumepata msiba mkubwa, Mzee wetu Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu amefariki dunia, amefariki dunia katika hospitali jijini Dar es Salaam ambako alikuwa amelazwa, niwaombe Watanzania tulipokee hili, tumepata msiba mkubwa na tuendelee kumwombea Mzee wetu Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa ambaye ametangulia mbele za haki, taarifa zingine zitaendelea kutolewa lakini Mzee Mkapa hatunaye tena," alisema Magufuli katika taarifa yake kwa Taifa.

Taarifa hiyo ya maombolezo ya Rais Magufuli, ilipokelewa kwa masikitiko makubwa na wadau wa soka nchini ambapo aliyekuwa Waziri wa Michezo wakati harakati za ujenzi wa Uwanja wa Taifa zikianza, Mudhihir Mohamed Mudhihir, alikuwa mingoni mwa walioguswa na msiba huo.

"Nakumbuka kwanza, alituagiza kutafuta eneo zuri litakalotosha kujenga uwanja, na Wachina waliposema wataujenga kwa gharama ya Sh. bilioni 80, aliongea nao na kufikia makubaliano na uwanja kujenga, hakika alikuwa msikivu na hata mawaziri wake walipoteleza aliweka mambo sawa na mambo kuendelea," alisema Mudhihir.

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Soka nchini (FAT) kwa sasa TFF, Ismail Aden Rage, alisema: "Mkapa alikuwa mwanamichezo wa kweli, enzi za FAT kulitokea tofauti katika uongozi hatua iliyosababisha tufungiwe na Fifa.

> **"Lakini nakumbuka aliwatuma mawaziri wake; Anna Abdallah na Prof. Sarungi (Philemon) kuongea na sisi na kuyamaliza na kisha tukarejeshwa Fifa, pia watu hawajui tu, lakini kuna wakati timu za taifa zilikwama nauli na yeye kuchangia."**

Nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) na mshambuliaji wa Aston Villa ya Ligi Kuu England, Mbwana Samatta, alisema: "Pumzika kwa amani Mzee Mkapa."

Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba Mohamed 'Mo' Dewji, yeye amemlilia Mkapa kwa kusema: "Inna lillahi wa inna ilayhi raji'un. Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwa hakika kwake yeye tutarejea.

"Bado ni vigumu kukubali kwamba Mzee Mkapa hatunaye tena. Pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa ujumla kwa msiba huu mzito. Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi. Tangulia Baba, nasi tunakuja."

Kwa upande wa uongozi wa klabu ya Simba umesema umepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa.

"Simba SC tunatoa pole kwa familia, ndugu, marafiki na Watanzania wote kwa msiba huu mkubwa kwa Taifa letu. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi. Amin."

Klabu ya Yanga kwanza ilisimama kwa dakika moja kabla ya safari yake ya Iringa kwenda kuivaa Lipuli FC kwenye mechi ya funga msimu Jumapili, ili kutoa heshima kwa kifo cha Mkapa.

Pili katika taarifa ya klabu hiyo ilieleza: "Tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benjamin William Mkapa. Tunatoa pole za dhati kwa Mama Anna Mkapa, familia, ndugu na Watanzania wote kwa msiba huu mkubwa. Bwana Ametoa na Bwana Ametwaa Pumzika kwa Amani Mzee Wetu."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002